SAUTI YA ILE ISHARA

. . . Maandiko. Nami ninatamani tungeweza tu kusimama tena kwa muda mfupi, tunaposoma kutoka kwenye Kitabu cha Kutoka. Na mlango wa 4 wa Kitabu hicho, katika Kitabu cha Kutoka, ningetaka kusoma kifungu cha 1 hadi cha 8.

> *Musa akajibu akasema, Lakini . . . hawataniamini, wala hawataisikia sauti yangu; maana watasema, BWANA hakukutokea.*
>
> *BWANA akamwambia, Ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako? Akasema, Ni fimbo.*
>
> *Akamwambia, Itupe chini; akaitupa chini, nayo ikawa nyoka; Musa akakimbia mbele yake.*
>
> *BWANA akamwambia Musa, Nyosha mkono wako, kamshike mkia; akaunyosha mkono wake, akamshika, naye akageuka kuwa fimbo mkononi mwake:*
>
> *Ili kwamba wapate kusadiki ya kwamba BWANA Mungu wa baba zao, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, . . . Mungu wa Yakobo, amekutokea.*
>
> *BWANA akamwambia tena, sasa tia mkono wako kifuani mwako. Akautia mkono wake kifuani mwake: naye alipoutoa, kumbe! Mkono wake ulikuwa una ukoma, umekuwa mweupe kama theluji.*
>
> *Akasema, Tia mkono wako kifuani mwako tena. Akautia mkono wake kifuani mwake tena, na alipoutoa kifuani mwake, kumbe! Umeirudia hali ya mwili wake.*
>
> *Basi itakuwa, wasikuposadiki, wala kusikiliza sauti ya ishara ya kwanza, wataisikiliza sauti ya ishara ya pili.*

2 Na tuombe. Bwana Yesu, Mungu usiyebadilika, usiyeshindwa, unayedumu yeye yule jana, leo, na hata milele. Wala Wewe hubadiliki, nasi tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo. Sasa libariki Neno Lako, na kusomwa kwa Neno Lako, moyoni mwetu. Na jalia tuwe na imani ya kukuamini Wewe. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

Ketini.

3 Sasa, ninyi ni moja ya makusanyiko mazuri sana niliyopata kuhubiria. Nami sisemi hayo kwa kusema tu. Ni kweli. Na sasa kwa namna fulani ninataka kuchukua wakati wangu kidogo, usiku wa leo, na kuweka mazingira haya. Kwa hiyo, kusudi la kufanya hivi, nipo hapa kuwasaidia. Na kama siwezi kuwasaidia ama kuwafanyia jambo fulani, vema, kuifanya mizigo ya maisha kuwa rahisi kidogo kwa ajili ya Wakristo, na kumleta mwenye

dhambi kwa Kristo, mimi ni mshindwa kabisa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Na kwa kweli ninataka kuwa baraka kwa Mungu, kwa kuwa Yeye ndiye nguvu zetu na uhai na msaada wetu.

4 Sasa katika kufundisha jambo hili, ninataka kuninii ili kwamba mfahamu. Unaona, yapo baadhi ya mambo yanayokuja wakati mwingine, ambayo ni ya ajabu sana, hata watu hawayapati vizuri. Na ninafikiri ingefaa kama tunalifanya jambo hilo wazi, dhahiri.

5 Watu wengi, kama vile sisi. . . kama huelezei uponyaji wa Kiungu. Sasa wakati mwingine Ndugu Roy, labda, mnamo dakika chache, anasema jambo hilo. Bali watu ndio ambao hawajui jinsi tu ya kushikilia uponyaji wa Kiungu, na hasa wakati a—adui anapokuja, mbona, unge—ungeweza kushindwa vita, kwa urahisi sana.

6 Mara nyingine wakati watu wanaposhikwa na ugonjwa baada ya kuombewa, wanafikiri, "Hiyo ni vit-. . . La, nimeupoteza." Hiyo ndiyo ishara kwamba umeupata. Unaona? Unaona, hiyo, hiyo ndiyo ishara yako. Kama hujui tu. . . kama humjui adui wako, unawezaje kumjua kwa dakika thelathini tu kila usiku katika ibada tano ndogo, kisha unaondoka unaenda mahali pengine?

7 Moja ya siku hizi, ninaamini Bwana. . . wakati ule ufufuo mkuu umetulia kote nchini. Nimemwomba Bwana, kama ni mapenzi Yake, anijalie kupata hema, nipige hema, wala isitubidi kukodisha chochote. Nami nifanye ibada ya asubuhi kwa ajili ya mafundisho, pamoja na wachungaji na kadhalika, labda toka saa nne hadi saa sita; alasiri, maelekezo juu ya uponyaji; na halafu usiku huo, kuwaombea wagonjwa. Siku baada ya siku, kwa majuma kadhaa. Na halafu bila ya kuwa na ibada za Jumatano usiku, ama ibada za Jumapili, kuingiliana, ama chochote kile. Jumapili alasiri tu, kusudi tusiingilie ibada iliyosalia, na hivyo kumruhusu kila mtu anayetaka kuja aje. Tuwaombee wagonjwa. Na ibilisi akirudi, ama akisema jambo lolote, basi tunaweza kuingia na kulichunguza hilo, na kuona ni kitu gani hasa kinachotendeka, mnaona.

8 Nafikiri hilo lingeweza kuwa ni baraka halisi kwa majirani, kwa wachungaji na wale wote ambao wangewajua. Wanaamini hili. Wanaliamini kabisa, vinginevyo wasingekuwa wakihubiri Biblia. Mwaminio yeyote wa Biblia, mwaminio halisi wa Biblia, huitikia kila moja ya ahadi hizi za Mungu kwa "amina." Hiyo ni kweli.

9 Kama huwezi kuliamini lote. . . Unasema, "Vema, ninaamini *hili*, bali sijui kuhusu *Lile*." Una mfasiri yule yule ambaye Hawa alikuwa naye. Alijaribu. . . Alijaribu kulifasiri kwa Hawa, "Loo, *hili* ni kweli, na *lile* ni kweli, na, loo, *hilo* kweli ndilo, lakini hakika Mungu. . . "

10 Mungu alisema hivyo, na kila Neno! Hakuna hata Neno moja wala sehemu Yake moja inayoweza kukosekana, kutokubalika. Usipolikubali kwa moyo wako wote, kila sehemu yake, basi afadhali usianze hata kidogo. Unaona?

11 Kumbuka, ilikuwa ni kifungu Chake kimoja kidogo cha maneno, kilichopinduliwa tu, ambacho kilisababisha kila ugonjwa, kila huzuni ya moyoni, kila kifo, kila kitu. Kilisababisha yote. Kwa kutokuamini tu kifungu kimoja kidogo cha maneno, kulisababisha yote haya, je! unafikiri kukiuka tu maksudi kifungu kimoja kidogo cha maneno kutakurudisha? Wakati, watu hawakubali nusu Yake, mara nyingine, halafu wanajiita Wakristo. Unaona? Unaona?

12 Ni sawa, kila sehemu Yake ndogo, linapaswa tu kuwekwa pamoja. Na kuna Mmoja pekee anayeweza kufanya jambo hilo, huyo ni Roho Mtakatifu, kwa kulifasiri kwa kutimiza Kwake Mwenyewe kile alichosema angefanya. Hiyo ndiyo njia pekee nijuayo. Sasa ninii yetu . . .

13 Nitazungumza nanyi usiku wa leo, ama kufundisha, kwa—kwa dakika chache, juu ya somo la . . . *Sauti Ya Ile Ishara*.

14 Je! mlitambua, Musa alisema pale, yeye ataninii . . . “Hawataisikia sauti yangu. Watasema, ‘Bwana hakukutokea.’”

Mungu akamwambia basi, kasema, “Sasa ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako?”

15 Akasema, “Mbona, ni fimbo, mkwaju; ni ufito tu uliokauka, fimbo ya mchungaji, kitu kama hicho.”

16 Kasema, “Itupe chini.” Akaitupa, nayo ikageuka ikawa nyoka. Akaitwaa tena, ilikuwa nyoka . . . ama fimbo tena.

17 Ndipo akasema, “Tia mkono wako kifuani mwako.” Naye akautoa, ulikuwa ukoma. Ndipo akaurudisha tena, akautoa, ulikuwa umeponywa. Akasema, “Sasa, wasipoisadiki sauti ya ishara ya kwanza, wataisadiki sauti ya ishara ya pili.”

18 Sasa je! uliona jinsi Mungu anavyofanya jambo hilo, Mungu asiyebadilika? Je! yeyote wenu anaweza akakumbuka kule Arkansas, yapata miaka kumi na mitano iliyopita, wakati Sauti ya ile ishara ya kwanza, ilipoahidi Sauti ya ishara ya pili? Unaona? Nilisema, “Hiyo itakapotimia, hakuna mtu atakayeweza, isipokuwa awe ni asiyeamini kabisa, maana itatambua na kujua kile alicho mtu, na inaweza kumwambia mambo yake.” Kwa hiyo yeye ni ninii . . . Ni wangapi wanaokumbuka ule unabi- . . . hilo likitabiriwa huko nyuma miaka kadhaa iliyopita, wanaohudhuria mkutano, na akasema itatimia? Malaika wa Bwana alisema, “Itakuwa kwamba hata utajua siri zilizo moyoni mwao.” Ni wangapi wanaojua jambo hilo? [Kusanyiko linsema, “Amina.”—Mh.] Hayo yalitabiriwa miaka mingi iliyopita, unaona, wakati ile ishara ya kwanza ilipokuwa ikitenda kazi.

19 Sasa, tukio letu liko huko mbali jangwani, juu ya nabii mtoro. Musa alijua ya kwamba alikuwa ameinuliwa ili kuwakomboa Israeli; alikuwa amejifunza jambo hilo kutoka kwa mama yake. Kwamba mama . . . Alikuwa mtoto aliyepaswa. Na—na Yakobedi na—na mumewe walikuwa wameomba ya kwamba Mungu atume mkombozi, naye huyo hapo akazaliwa katika familia yao, "mtoto aliyepaswa." Tunajua hadithi hiyo. Na sasa wakati alipolelewa, alichukua njia ile ile ya kufunzwa kwa ajili ya kazi hiyo, kama vile ambavyo tungeweza kumfundisha mtu leo, moja kwa moja hadi shuleni, kwenye shule nzuri kuliko zote.

20 Kama mtu alifikiri tulikuwa na—na wito maishani mwake, ni kitu gani kingetukia? Wangempeleka huko Bob Jones, ama mahali fulani, ama kwenye baadhi ya shule kuu, na kumpatia aina ya elimu ya juu sana angeweza kupata. Na hilo ndilo jambo baya zaidi wangaliweza kufanya. Hilo ndilo jambo baya zaidi lingaliweza kufanywa. Wakati mtu anaposema, "Mimi ni Ph.D., LL.D.," hilo linamweka tu mbali sana na Mungu, kwangu mimi. Unaona? Mungu haninii, si vitu vyote hivyo hapo. Mungu ni Mungu, rahisi, mnyenyekevu. Unajua, unatembea . . . Wanajaribu kupasua atomi, na—na kujaribu kusema jinsi unavyopaswa kufanya jambo hilo, na halafu wanatembea juu ya unyasi ambao hawajui kitu kuuhusu. Hiyo ni kweli. Unajipeleka mbali tu na Mungu kwa mambo hayo. Si kwamba ninaunga mkono ujinga, sasa, msifikiri hivyo.

21 Lakini ninajaribu kuwaambia ya kwamba Mungu hajulikani kwa elimu. Mungu anajulikana kwa imani. Imani, unamjua Mungu, na hiyo pekee, na imani tu. Inakubidi tu kuwa na kitu cha kuwekea msingi imani, kwa kuwa si kitu kisicho na msingi; hilo ni Neno Lake. Naye Musa alienda shuleni, nao walimfundisha zaidi na zaidi, kwa sababu, hapana shaka, walidhani ya kwamba angekuwa mwanajeshi mkuu sana. Nayo historia inatwambia yeye alikuwa mwanajeshi mkuu sana, aliweza kuteka majeshi ya Misri na—na kuwa Farao wa Misri, na kuwaweka watu huru, na kuwarudisha kwenye nchi ya uenyeji wao ama kuwaacha waiteke Misri. Sasa hivyo kweli ndivyo walivyodhani ingetukia. Na kwa hiyo walimfunza, na—na hata angeweza kuwafundisha wanazuoni hekima kidogo. Alikuwa mwerevu kweli na msomi. Lakini hiyo haikuwa njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo. Na wakati alipoona kwamba imeshindwa, akaghadhabika.

22 Na hivyo ndivyo makanisa yanavyofanya leo. Wakati wanapoona, mpango wao wa elimu, huwezi kumwelimisha Mungu, mtu kwa Mungu, huwezi kumundia madhehebu amjue Mungu. Mungu ana njia ya mtu kupitia, na hiyo ndiyo njia pekee Mungu anamtambua kwayo, hiyo ni chini ya Damu. Wala huwezi kufanya hivyo kwa kusema, "Sote tutakuwa Methodisti. Sote tutakuwa Baptisti. Sote tutakuwa Waassemblies. Sote tutakuwa kanisa la Mungu. Sote tutakuwa Umoja. Tutakuwa *hili*." Hilo

halitamridhisha Mungu, kwa sababu, mpango Wake, kwamba hatuna budi kuzaliwa mara ya pili na kuja chini ya Damu. Na kwa hiyo mipango ye—yetu ni ya kujibunia tu, nayo imeanza, kushindwa, na daima itashindwa mpaka tutakapoirudia njia ya Mungu ya kutekeleza jambo hilo. Hiyo ndiyo njia pekee ambayo Mungu anaijua, ni chini ya Damu. Hapo ndipo anapopita juu.

23 Wengi wenu walikuwa kule chini hivi majuzi usiku, ama Jumapili alasiri, nadhani, chini kule wakati nilipohubiri juu ya *Ile Ishara*. Ishikilie Ishara mbele yako. Ni wangapi waliokuwa kule chini, hebu tuone mikono yenu? Vema, nilifikiri kulikuwa na kundi kutoka hapa lililokuja kule chini. Na, hiyo Ishara, hicho ndicho kitu pekee ambacho Mungu hutambua, na hiyo Ishara haina budi kuwako la sivyo agano hata linabatilishwa. Ni Ishara tu! Na hiyo Ishara ni Roho Mtakatifu.

24 Sasa tunaona ya kwamba Musa, baada ya kufanya jambo hili, alighadhabika. Kwa hiyo alikimbia tu, akaondoka Misri na akaenda huko—huko jangwani, na huko tunaona ya kwamba alimwoa msichana wa Kushi, na akapata mwana jina lake Gershomu. Na siku moja wakati alipokuwa akitembea kandokando ya—ya njia ya zamani aliyoijua kwenye sehemu za mbali huko jangwani, akiwachunga kondoo, vema, alivutiwa na tamasha lisilo la kawaida.

25 Na Mungu si wa kawaida kabisa, Yeye hufanya mambo kwa njia isiyo ya kawaida kabisa; kinyume kabisa na sayansi, kinyume mno na elimu, kinyume kabisa mara nyingine na theolojia ya mwanadamu, kinyume tu na hiyo. Mungu hufanya jambo hilo kuonyesha tu ya kwamba Yeye ni Mungu. Na, ili kufanya jambo hilo, inambidi kumchukua mtu asiyejua chochote kuhusu mambo haya, ili apate kutenda kazi kupitia kwa mtu huyo.

26 Wakati Yesu alipokuja, kwa nini hakumchukua Kayafa, makuhani waliokuwa wamefunzwa na wako tayari kwa ile kazi? Alishuka akaenda kuchukua watu ambao hata wasingeweza kuandika jina lao, "wasio na elimu wala maarifa," Biblia ilisema ndivyo walivyokwa. Maana, Mungu huchukua kitu duni kufanya kitu fulani kutokana nacho. Unaona?

27 Na wakati wowote unapofikia mahali unapojisikia ya kwamba wewe si kitu, ndipo basi karibu uko tayari kabisa kumjia Mungu. Unapo—unapofikia mahali ambapo hujui kitu, bali unataka kujua kitu, basi Yeye atajifunua Mwenyewe kwako.

28 Sasa, angalieni wakati jambo hili lisilo la kawaida, kamwe halikuwa limetendeka ulimwenguni, tunavyojua. Ilikuwa tu ni wakati wa kule kutoka. Kutoka kulikuwa kumekaribia, na, wakati, *kutoka* maana yake ni, "kutolewa, kutolewa nje."

29 Na sasa tunaona ya kwamba, kwa kawaida, kwenye hizo njia panda za kutoka, yasiyo ya kawaida huanza kutukia. Ninaamini tupo hapo tena. Ninaamini tupo pale, kwenye kutoka kwa

Bibi-arusi, kwenda kumlaki Bwana Arusi. Ninaamini kutoka kumekaribia.

30 Na kutoka huku, kutolewa kutoka—kutoka Misri, kurudi kwenye nchi ya uenyeji wao walikoahidiwa kuja, kulikuwa kumekaribia sana, na ilibidi Mungu kumwelimisha tena mtu Wake. Kumbukeni, Musa alikuwa ameelimishwa kwa muda wa miaka arobaini, akipata shahada zake zote za udaktari na kila kitu, na ilimchukua Mungu miaka mingine arobaini tu kutoa ndani yake kile ambacho elimu ilikuwa imetia ndani yake. Miaka arobaini jangwani; kipindi kilichotumika, kukitoa, ndicho kilichotumika kukitia ndani.

31 Ndipo, na kitu hiki chote kikubwa kilipomtoka, Mungu alimtokea katika mfano wa kijiti kilichowaka moto. Sasa nitawaonyesha ya kwamba kilikuwa kimemtoka. Sasa, kama sivyo, sasa Musa akiwa mwa—mwanasayansi, angalienda kuchuma baadhi ya majani hayo kutoka mtini, na kuyapeleka kwenye maabara ili yapate kuchunguzwa, apate kuona ni kemikali ya namna gani yaliyonyunyiziwa nayo, hivi kwamba mti huo ungeweza kuwaka moto wala usiteketee. Unaona?

32 Kwa sababu, sasa, Wamisri walikuwa ni watu werevu, wa kisayansi, werevu zaidi katika sayansi kuliko tulivyo leo. Inathibitisha hilo. Wangaliweza kutia dawa ya kuhifadhi maiti ambayo ingali inaonekana haijabadilika leo hii. Hatuwezi kufanya hivyo. Kujenga piramidi. Tusingeweza kufanya hivyo. Unaona? Mambo waliyokuwa nayo yalikuwa yamepita sayansi yetu leo kwa mbali sana.

33 Na kwa hiyo Musa alikuwa amefunzwa katika hekima yote, kwa hivyo hiyo ilimfanya kuwa mwanasayansi. Kwa hiyo, unaona, wakati alipokuja Mbele ya kijiti hiki, alijua kijiti hicho kilikuwa na yale aliyopungukiwa nayo.

34 Laiti tungaliweza kufanya jambo hilo leo, laiti tungaliweza tu kujua tukio hili la ajabu la Mungu lina yale tuliyopungukiwa nayo katika madhehebu yetu. Yale ambayo mfumo wetu wa elimu umepungukiwa nayo, Mungu anayo katika tukio la ajabu la Uwepo wa Kristo. Hilo ndilo tunalohitaji.

35 Sasa, tunaona, kutoka huku kukiwa kumewadia, Mungu alikutana na Musa na kumwambia kile kitakachotukia, na akampa ishara mbili. Na kila ishara ilikuwa na Sauti, Sauti ya ishara.

36 Kila ishara inayotoka kwa Mungu hufuatwa na Sauti. Kila wakati Mungu anapotoa ishara ya kweli, ipo Sauti inayoifuata. Wakati ukiona namna fulani ya tukio la ajabu likitokea, na unaliangalia likipamba moto, wala halibadiliki kuwa kitu fulani, basi kamwe halikutoka kwa Mungu. Unaona? Mungu haonyeshi tu ishara kwa kuonyesha tu ya kwamba Yeye ni Mungu. Ipo Sauti inayoifuata ishara hiyo.

37 Sasa, kwa msaada wa Mungu, tutaona jambo hilo katika Maandiko usiku huu, na tuone kama hiyo ni Kweli. Unaona? Hapa kijiti kilichowaka moto kilikuwa ni ishara kwa Musa, hiyo ilikuwa ni ishara, na ilitolewa kwa . . . naye alisikia Sauti kutoka katika kile kijiti.

38 Sasa angalia, Mungu kamwe habadilishi mpango Wake. Yeye kamwe halazimiki kughairi Maneno Yake. Uamuzi Wake wa kwanza ni mkamilifu.

39 Mimi ninaweza kutoa uamuzi, nitasema, "Vema, ni—nilikosea, unaona." Mimi ni mwanadamu. Unaweza kutoa uamuzi fulani na inakulazimu kughairi.

40 Sayansi hutoa uamuzi kisha ikaughairi. Je! mlijua hilo? Wanaweza kuthibitisha kisayansi kwamba jambo fulani ni kweli, na baada ya kitambo kidogo wanathibitisha kisayansi kwamba si kweli, bali hawatakubali makosa yao. Hawatakubali yao.

41 Sasa, mwanasayansi Mfaransa, yapata miaka mia sita iliyopita, ama kitu kama hicho, akifingirisha tufe kwa mwendo fulani kuizunguka dunia, ikiwa ni ardhi; ama—ama miaka mia mbili iliyopita, ninaamini ndivyo ilivyokuwa, ama mia tatu, kitu kama hicho. Hata hivyo, alithibitisha kisayansi, kwa kuinua mpira huu, katika mwendo huo . . . Kama—kama mtu angeenda kwa mwendo wa kasi mno wa maili thelathini kwa saa, kitu chochote kikienda juu ya nchi kwa mwendo wa maili thelathini kwa saa, mvutano ungepoteza nguvu zake na kitu hicho kingeondolewa ardhini. Unafikiri sayansi hurudi nyuma na kutambua jambo hilo? La. Wanasonga mbele zaidi na zaidi. Unaona?

42 Bali wahudumu daima wanajaribu kurejea kwenye kile mtu mwingine alisema, huko nyuma yao kabisa, badala ya yale Mungu aliyosema yafanywe. Tunaukwea mti wa Imani. Mnaona?

43 Na Mungu kamwe habadilishi mpango Wake. Unaweza kutulia kwa dhati juu ya yale Mungu asemayo kwa mara ya kwanza. Daima inampasa kudumu na Hilo. Hawezi, Hawezi, wala kamwe hajawahi kufanya hivyo, wakati wowote, kulibadilisha. Kwa sababu, kama akibadilisha, basi Yeye—Yeye ana kikomo kama tulivyo; anakosea, hana budi kuomba msamaha na kurudi nyuma. Bali Yeye ni chemchemi ya hekima yote, chimbuko la nguvu zote; asiye na kikomo, aliyepo kila mahali, ajuaye yote, mwenye nguvu zote. Unaona, Yeye ni mwenye haki, Yeye ni Mungu. Kama Yeye si mambo hayo yote, basi Yeye si Mungu. Bali inambidi awe hivyo apate kuwa Mungu.

44 Sasa, Mungu kamwe hajawahi kutumia mpango fulani uliobuniwa na mwanadamu kumheshimu Yeye, ila tu kwa kuufedhehesha. Mungu daima hutumia mtu mmoja binafsi, mmoja tu; si shirika kamwe, si dhehebu kamwe. Yeye humtumia

mtu mmoja binafsi, kwa kuwa sisi tunatofautiana, sote, mmoja kwa mwingine. Kamwe hakujawahi kuwa na manabii wawili wakuu duniani kwa wakati mmoja. La hasha. Unaona, Yeye hafanyi hivyo, kwa sababu Yeye husema tu na huyo mmoja. Huyo mmoja akishaondoka, Yeye humwinua mwingine kunena wakati huo. Kumbukeni, huo daima umekuwa ndio mpango Wake.

45 Sasa tunaona hapa, kile kijiti kinachowaka moto kilikuwa ni ishara. Ilitolewa kuvutia usikivu wa Musa.

46 Sasa hiyo ndiyo sababu ya Mungu kutoa ishara, ni kuvutia usikivu wa watu. Hilo ndilo kusudi la ishara, ni kuvutia usikivu. Na tukipitia kwenye Maandiko hapa chini, tunapofundisha Hilo sasa kwa dakika chache, na tuone kama hilo si kweli, ya kwamba Yeye hutoa ishara hizi kuvutia usikivu. Ndipo basi wakati anapopata usikivu wa watu, ndipo Sauti ya ishara inaanza kuzungumza. Yesu aliwaponya wagonjwa, apate kuvutia usikivu, unaona, ndipo alipoanza kuhubiri. Unaona, hizo daima, huvutia usikivu.

47 Kile kijiti kilichowaka moto kilipewa Musa, kuuvutia usikivu wa nabii mtoro, naye akageuka apate kuona kilikuwa ni kitu gani. Ndipo hiyo ishara ikatoa Sauti. Ishara yenyewe ilitoa Sauti.

48 Sasa hizi sauti na ishara ni za kuwatahadharisha watu juu ya Neno la Mungu, kwamba liko tu tayari kuthibitishwa. Daima ishara ni ya kuvutia usikivu, watu.

49 Sasa wengi wenu ninyi wasomaji wa Biblia, na mna— mnawazia sasa juu ya vifungu mbali mbali katika Biblia, na tutaendea baadhi yake, kwamba, ishara inapotolewa, huvutia usikivu wa watu, kwa maana Mungu yuko tayari kunena. Anataka kusikilizwa. Anataka mtu atakayesikiliza yale atakayosema. Unaona? Sasa, daima Yeye hufanya hivyo. Neno Lake linawatahadharisha juu ya . . . Ishara hiyo ni tahadhari, kuvutia usikivu wa watu, kwamba Neno liko tayari kunena.

50 Sasa angalia, Yeye atanena kwa Neno Lake lililoahidiwa, jambo alilosema kwamba atafanya. Angalia, "Nimesikia, Nami ninakumbuka ahadi Yangu. Nilisikia vilio vyao huko Misri; ninakumbuka kile nilichomwahidi Ibrahimu."

51 Unaona kile atakachofanya? Alivutia usikivu wake, sasa yeye analo Neno Lake, atalitoa kwa nabii, Musa. Kwa maana, hiyo ilikuwa, ndivyo ilivyo sasa, na daima itakuwa hivyo, ndiyo njia Yake ya kuzungumza. Hivyo ndivyo alivyofanya hapo mwanzo, hivyo ndivyo anavyofanya sasa. Yeye hufanya vivyo hivyo daima. Mnaona? "Neno linamjia nabii." Naye Musa alikuwa ndiye nabii mhusika, na sasa inambidi kutabiri ya kwamba atawapandisha Israeli. Hakusema jinsi atakavyofanya jambo hilo, bali alikuwa yuaenda kuwatoa Misri. Na, basi, Yeye alikuwa amesikia vilio vyao, na kuugua kwao, na maombi yao. Walikuwa tu wakimngojea Mungu . . . Mungu alikuwa

akiwangojea. Yeye alikuwa na nabii Wake huko nje jangwani, bali alikuwa tu akiwangojea watu hao wamwite atende kazi.

52 Ninaamini ana jambo lile lile leo, analingojea kanisa Lake limwite aje jukwaani, ili Yeye atende kazi. Ahadi ya leo iko tayari, bali hana budi kuwafanya watu waombe na kuugua kama walivyokuwa wakifanya zamani zile, ndipo atajitokeza jukwaani. Mnaona?

53 Musa alikuwa huko nje jangwani, akingojea kule kwa muda wa miaka arobaini. Watu hao walikataa ile—ile ishara, jambo alilofanya kule, kumwua yule Mmisri; haikuwa ni njia ya Mungu, kwa hiyo alimweka huko nje jangwani na—na kumwelimisha tena sasa juu ya tukio hilo la ajabu sana, na sasa yuko tayari. Ndipo Mungu akasema, "Nilisikia kuugua kwao, nimeona kuugua kwao, wanyapara wao wakiwacharaza, nami ninakumbuka ahadi Yangu." Amina. Unaona, Yeye yuko tayari kunena sasa, ameweka kila kitu katika utaratibu. Sasa anaonyesha tukio la ajabu sana linalovutia usikivu wa nabii huyo.

54 Wakati nabii aliposhuka kwenda kule, alionyesha tukio hilo la ajabu sana, kwa maana yeye alikuwa sauti ya Mungu. Mtu angewezaje kuchukua mavumbi na kuyatupa, na kusema BWANA ASEMA HIVI; hakuna kiroboto hata mmoja nchini, na, saa kadhaa baadaye, kila kitu kimejaa viroboto? Hakuna nzi yeyote popote, hata kidogo, naye angesema, "Na kuwe na nzi"; na, muda si muda mnajua, nzi mkubwa mchafu anaanza kuruka pale, nao walikuwa wakiwafurikia watu kila mahali. Ni nani, ni mtu gani angaliweza kufanya jambo hilo? Ilikuwa ni Mungu akimtumia nabii huyo, akilifanya neno Lake kuwa ishara, kutoa wito, "Tunatoka Misri."

55 Pale, angalieni kwa makini sana sasa. Yeye atazungumza, kwa hiyo hana budi kuvutia usikivu kwa ishara, na sauti ya ishara ndiyo atakayosema. Neno Lake, Neno Lake lililoahidiwa litathibitishwa sasa. Unaona? "Nilitoa ahadi ya kwamba nitawatoa kwa mkono wenye nguvu; ningeonyesha nguvu Zangu katika nchi hiyo," na lolote atakalofanya. Sasa, Yeye alitoa ahadi kwa Ibrahimu, huyu hapa akiwa tayari kuitimiza. Kwa hiyo, Yeye anatoa ishara, Nguzo ya Moto ikiwa huko nyuma kwenye kijiti kilichowaka moto, Naye anamwambia Musa, "Sasa utakuwa msemaji Wangu. Shuka uende kule, na Mimi nitakuwa pamoja nawe."

56 Na alipofika kule, ndipo lile Neno lililoahidiwa, ambalo alikuwa ameahidi, lilithibitishwa. Hiyo ilikuwa ndiyo Sauti ya ile ishara. Mnalipata sasa? Angalieni, "Nimesikia kuugua kwao. Ninakumbuka ahadi Yangu."

57 Mungu kamwe habadiliki. Yeye daima hufanya jambo hilo kwa njia ile ile. Kuja kwa nabii ni ishara ya kwamba Mungu yuko tayari kunena. Je! mlininii. . .Sasa yachunguzeni Maandiko.

Mnaona? Biblia ilisema, Mungu alisema, Mwenyewe, Yeye "hakufanya lolote mpaka alipolifunua kwa manabii Wake." Hiyo ni kweli. Yeye anafanya hivyo kupitia kwao, kwa sababu linamjia yeye. Hao ni watumishi Wake, mnajua. Vema.

58 Kuja kwa nabii ni ishara inayopuuzwa na watu, kila mara. Watu huipuuza. Hawaipati hata, kwa namna fulani, isipokuwa iwe ni wale ambao macho yao yamefunguliwa kuliona. Wale walioteuliwa kuliona, huliona. Bali kule kuja kwa nabii kulikuwa ni ishara ya kwamba Mungu yuko tayari kunena, maana, kama Mungu hatanena, nabii asingekuwepo duniani. Sasa kumbukeni jambo hilo, asingekuwepo duniani isipokuwa Mungu alikuwa tayari kunena. Na hivyo ndivyo anavyonena, ni kupitia njia hizo. Mungu asiyebadilika kamwe hajawahi kufanya jambo hilo kwa njia nyingine yoyote. Angalia.

59 Hii daima ndiyo njia ya Mungu ya kuifanya Sauti Yake ijulikane kwa watu Wake. Yeye humtuma nabii Wake na kumpa ishara; na halafu anachukua Sauti Yake ambayo imenenwa hapo awali, kwenye Neno Lake, na kuithibitisha kwa mtu huyu. Nao wanajua ya kwamba ni Sauti Yake kwa maana ndilo Neno lililoahidiwa la siku hiyo. Loo, laiti watu wangaliweza tu kuona jambo hilo. Laiti wangalitulia tu kwa muda kidogo na kutambua jambo hilo. Unaona, hakuna njia ya kuwafanya waliamini; hakuna ninii—hakuna njia, mtu. Mungu Mwenyewe hawezi kufanya hivyo, kuwafanya watu waliamini. Hawana budi kuliamini. Na kama hakuna kitu pale cha kuaminia, wanawezaje kuamini, unaona, haijalishi unafanya nini?

60 Biblia ilisema, "Walakini ajapokuwa amefanya miujiza mingi sana, hata hivyo hawakuweza kuamini," kwa sababu, Isaya alitangulia kuliona, na kusema, "Wana masikio wala hawawezi kusikia, macho wala hawawezi kuona." Na hata hivyo alikuwa ndiye Masihi kikamilifu, alifanya yale hasa Masihi aliyosema. Nao wakasema, "Mtu huyu huyavunja tu makanisa. Na, Yeye, hatujui anatoka wapi." Mnaona? Hiyo si ni ajabu kwamba wangefanya hivyo? Bali Biblia ilisema ya kwamba wangefanya hivyo.

61 Na Biblia ilisema pia, katika siku hii wangefanya jambo lile lile. "Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasingiziaji, wasiojizuia, wenye kudharau walio wema; wenye mfano wa utauwa, lakini wangekana Neno lililothibitishwa, Nguvu zake, Ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kadhalika; hao nao mjiepushe nao. Kwa maana hawa ndio wanaounda mashirika ya wanawake, na wanaingia nyumba kwa nyumba, na kuwaongoza wanawake wajinga waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi, wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa Kweli." Unaona? Sasa, hilo limetabiriwa, na hilo halina budi kutimia kwa sababu ni BWANA ASEMA HIVI. Angalia, "Lakini upumbavu wao utakuwa dhahiri, kama vile Yane na Yambre, katika siku za mwisho."

62 Sasa daima akifanya Sauti Yake ijulikane kwa watu Wake, kwa ishara Yake ya nabii. Sasa ninazungumza juu ya Musa, hapo ndipo ninaporejea, ndipo tuone mahali tulipo. Neno la Mungu hudhihirishwa kwa Sauti ya ishara.

63 Sasa ishara iliyoahidiwa kwa ajili ya siku hii, inapofanywa mbele za watu, na kisha Maandiko yaliyoandikwa yanajitokeza, ndiyo Sauti ya ishara hiyo. Kama haitoi Sauti ya Kimaandiko, basi kaa mbali nayo, unaona, si Mungu. Maana, Mungu hawezi kuahidi Hili kwa ajili ya siku hii, na kusema "Vema, ndilo *hili*." Unaona, Mungu hawezi kufanya hivyo. Mungu hawezi kuahidi jambo kwa siku fulani, na kusema, "La, la, si—sivyo. Si—sitafanya hivyo. Hilo lilikuwa ni la siku nyingine." Kile anachoahidi, hana budi kudumu nacho, na ishara halisi ya Kimaandiko ndiyo Sauti ya Kimaandiko.

64 Ishara ya Musa, ambayo yeye aliiona, ilikuwa ni Mungu katika nurulimwengu. Na basi wakati alipofanya hivyo . . .

65 Na je! mtu yeyote anaijua ile ishara ya kale ya Kiebrania, hata kabla Biblia haijaandikwa? Ilikuwa ni umbo la pembetatu, ama nurulimwengu yenye umbo la yai, kweli kabisa, ile Logos. Sasa, Daktari Lamsa ana hiyo kwenye Biblia yake, juu ya jalada upande wa nje.

66 Sasa tunaona ya kwamba Musa alivutiwa na ishara hii, na ishara hii ilinena na Musa kwa sauti ya Kimaandiko. Unaona, ile ishara ilimvutia. Ndipo akasema, "Ninakumbuka ahadi Yangu, Nami nimeshuka kuja kuwakomboa. Nami nitakutuma kama msemaji. Wewe shuka uende kule." Musa alitoa visababu vyake, bali Mungu alimtuma, hata hivyo.

67 Sasa, Yeye, hiyo ndiyo njia Yake ya kufasiri Neno Lake. Nabii, katika Maandiko, hana budi kwanza kuwa mwo—mwonaji aliyethibitishwa. Haipaswi kabisa kuwa mtu yeyote anayejitokeza, aseme, "Mimi nina BWANA ASEMA HIVI," na huyo mwingine aseme, "Ninasema BWANA ASEMA HIVI." Manabii hawawekewi mikono na kufanywa manabii. Manabii wanachaguliwa tangu awali kwa ajili ya wakati huo. Biblia husema wakati watakapokuja, jinsi watakavyokuwa. Manabii wa—wanatumwa kutoka kwa Mungu. Wao ni huduma za Mungu, waliozaliwa.

68 Mungu alimwambia Yeremia, "Kabla hata hujazaliwa katika tumbo la mama yako, nilikuchagua kuwa nabii kwa mataifa." Unaona? Wananinii tu . . . Hilo linapaswa kuwa ndani ya mtu huyo kikamilifu. Ni ninii . . . Si yeye; ni karama kutoka kwake. Musa alizaliwa nabii. Yeremia alizaliwa nabii. Isaya, nabii. Yohana Mbatizaji, nabii. Mungu alikuwa amenena kuwahusu.

69 Na yale wasemayo hayana budi kuwa ni ya kweli. Na jinsi ambavyo watu watakavyojua kama wao ni wa kweli ama si wa kweli, yale Yeye asemayo hayana budi kuwa sahihi, kwa maana yale anayotabiri ndiyo kitambulisho cha wito wake kutoka kwa

Mungu, wakati Mungu anapothibitisha yale anayosema kuwa ni Kweli. Sasa hiyo ndiyo sababu ninajaribu kusema mambo haya usiku wa leo, kusudi mpate kufahamu. Mnaona? Sasa kama . . .

70 Biblia ilisema hapa, "Akiwemo mmoja miongoni mwenu, ambaye ni wa kiroho ama ni nabii, Mimi Bwana nitajitambulisha Kwake, katika maono, nitasema naye katika ndoto." Kisha anasema, "Kama nabii huyu akisema neno lolote na lisitukie, basi msiliamini." Sasa hilo ni jambo la busara kabisa. "Lakini kama asemalo likitimia, basi sikilizeni, basi hamna budi kumwogopa," kwa maana Yeye yuko pamoja naye.

71 Sasa tunaona, yale Musa aliyosema yalitimia. Unaona? Hilo lilimfanya mwonaji aliyethibitishwa. Hicho ndicho kilichokuwa kitambulisho chake, kwa maana aliyosema yalitimia. Alisema, "Mnamo wakati huu kesho kutakuwa na viroboto kote nchini," na wakaweko. "Wakati huu kesho kutakuwa na jambo *fulani*," na kukawa. Lazima litimie kikamilifu kabisa, si kwa kubahatisha tu.

72 Watu wengi sana leo, kama mtaruhusu jambo hili kwa muda kidogo tu. Wala mimi si hakimu wala . . . Ninatoa tu maoni ya binafsi. Watu wengi wameinuka, watu wazuri waliojazwa na Roho, nao wanajaribu, wanatoka . . . Labda Bwana aliwapa karama ya unabii.

73 Sasa, kuna tofauti ya maili milioni moja kati ya kipawa cha unabii na nabii. Unaona? Kipawa cha unabii hakina budi kupambanuliwa na watatu kabla hata hakijatolewa kanisani. Tunajua ni sawa na kunena kwa lugha, hakina budi kwenda mbele ya waamuzi watatu kabla hata hakijatolewa kwa kanisa.

74 Sasa tunaona, sasa kwa kuwa watu hawa wanatoka nje wakati mwingine, na ndipo watu wanaanza kuwaomba sana, "Loo, ndugu, utasema nini?"

75 Unaona, yeye anaenda kwa dhana, unaona, jinsi anavyojisikia, "Mbona, Bwana atafanya jambo *hilo*, BWANA ASEMA HIVI." Huo ni uongo, unaona. Wewe, wakati . . . Huwezi kusema BWANA ASEMA HIVI mpaka Mungu, katika lugha Yake Mwenyewe, amesema na wewe na kukwambia hivyo, ndipo si wewe unayesema jambo hilo, si dhana yako. Biblia ilisema ya kwamba kama nabii alifanya hivyo, alikuwa akienda kwa kukisia, huko ni kukisia, na *kukisia* ni "kujasiria bila mamlaka," yeye anakwenda kwa uamuzi wake.

76 Lakini unapomwona mtu akisema yale yatakayotukia, katika Jina la Bwana, na yanatukia siku baada ya siku, juma baada ya juma, mwezi baada ya mwezi, mwaka baada ya mwaka, basi unajua hilo linatoka kwa Mungu. Unaona? Hicho ndicho kitambulisho cha Mungu kwa mtu huyo, ya kwamba yeye ni mfasiri wa Neno lililoandikwa kwa ajili ya siku hiyo, kwa maana Mungu alimtuma mtu huyo kufanya jambo hilo.

77 Laiti makanisa yangalikuwa na mafundisho mazuri, makamilifu juu ya mambo haya, unaona, wangelifahamu jambo Hilo. Jambo tu ni kwamba, tunashika njia moja ndogo na kutimua mbio nayo kama wenda wazimu, yaani mtu anachukua tu jambo hilo moja na kulifanya jambo la burudani. Huko ndiko kila—kila dhehebu lilikotokea.

78 Kama Martin Luther angaliendelea hadi aufikie utakaso, sawa. Iwapo Wamethodisti wa Kiwesley wangaliendelea wakaingia katika Ubatizo wa Roho Mtakatifu na kurudishwa kwa karama, lote lingalikuwa ni kanisa moja kubwa la Bwana, wakati wote. Lakini watu wanashika jambo hilo moja dogo na kuthibitisha kwamba ni kweli, basi hao hapo wanakaa. Lakini, iliwabidi kufanya hivyo, Biblia ilisema hivyo ndivyo wangefanya. Unaona? Na inapaswa kuwa hivi, leo.

79 Ninatumaini ya kwamba darasa langu linafaha-. . .Je! mnafahamu ninalomaanisha? Inua mkono wako ili kwamba . . . Mnaona? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Na, kufahamu, yakupasa ufahamu. Ewe rafiki, Huu ni Uzima wako. Unaona? Huu ni Uzima wako. Naam.

80 Kitambulisho chake ni kwamba Mungu amemthibitisha mtu huyu kwamba ni mwonaji.

81 Sasa neno la Kiingereza, *nabii*, linamaanisha tu "mhubiri." Unaona? Mtu yeyote, kila mhubiri ni nabii, maana yeye anatabiri kitu fulani. Akihubiri Neno, chini ya uvuvio, anaitwa "nabii."

82 Lakini katika Agano la Kale, walikuwa zaidi ya hivyo, walikuwa ni waonaji. Unaona? Walikuwa ni watu waliosema mambo yatakayotimia, nayo yakatimia. Hilo lilimpa yeye haki za kuwa m—mfasiri wa Neno kwa ajili ya siku hiyo, kwa maana Mungu alichukua Neno la siku hiyo na kulifasiri, Yeye Mwenyewe, kupitia mtu huyo. Na hilo ndilo lililomleta duniani, yeye daima ni ishara, wakati nabii anapokuja duniani. Angalieni tu tunapolipitia, mwone kama sivyo. Yeye daima humtuma nabii Wake. Unapomwona nabii akijitokeza jukwaani, [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] kaa chonjo. Tunamtarajia mmoja aje sasa, mwajua. Ndipo wakati mtakapoona jambo hilo, hebu kumbukeni tu ni jambo fulani liko karibu kutukia. Huu ndio utambulisho wake, ndio Mungu analifasiri Neno Lake kwa yeye na kupitia kwake. Hesabu 12:6 inasema hivyo.

83 Na, kumbukeni, Biblia nzima iliandikwa na manabii. Kwa nini? Neno la Mungu liliwajia baada ya wao kuthibitishwa. Manabii kama vile Yashari, na baadhi yao ambao walitupiliwa nje, na manabii wengi ambao hawakuendelea; bali Mungu ana njia ya kusukuma mbele Neno Lake, wakati likiwa ni Kweli. Mungu hana budi kuuhukumu ulimwengu kwa kitu fulani.

84 Wakatoliki hapa, wao wanasema, "Yeye atamhukumu, atauhukumu ulimwengu, kwa kanisa." Kama hilo ni kweli, basi ni kanisa lipi? Kama ukisema, "Kanisa Katoliki." Ni lipi, la

Kirumi, Kiyunani, ama lipi? Unaona, yote yamesambaratika vipandevipande.

85 "Atauhukumu kwa kanisa la Kibaptisti." Basi vipi kuhusu kanisa la Kimethodisti? Unaona? Unaona, Yeye hawezi kufanya hivyo, kuna michafuko mingi mno. Watu wasingejua mahali walipokuwa.

86 Lakini Yeye alisema, katika Biblia, kama unataka kujua kile atakachowahukumu wa—watu nacho. Atauhukumu ulimwengu kwa Yesu Kristo, na Yeye ni Neno. Biblia, basi, ndiyo atakayowahukumia, Neno lililothibitishwa. Hiyo ndiyo njia ya Mungu ya kuhukumu kwayo, ni Biblia. Kwa hiyo haidhuru kanuni yoyote ya imani ama madhehebu yanasema nini, wewe dumu moja kwa moja katika Biblia hiyo, maana hiyo Ndiyo Kristo. Yohana Mtakatifu, mlango wa 1, inatwambia hivyo.

87 Angalia sasa, Biblia iliandikwa na manabii. Tunaona ya kwamba inasema ya kwamba, "Watu wa kale, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, waliiandika Biblia." Katika Waebrania 1, inasema, "Mungu, ambaye kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi alisema na baba zetu kwa manabii, katika siku hii ya mwisho kwa Mwanawe, Yesu Kristo." Unaona? Kwa maana Yeye alikuwa ni dhihirisho la Neno lote la nabii, Naye alikuwa utimilifu wa Neno. Neno lilikuwa ndani Yake, Neno lote. Yeye alikuwa *Imanueli*, "Mungu aliyedhihirishwa katika mwili."

88 Mungu alishuka katika umbo la Roho Mtakatifu, mbawa mbili kama hua akishuka na akaenda kukaa juu Yake, akisema, "Huyu ni Mwanangu ninayependezwa kukaa ndani Yake." Sasa tafsiri ya Mfalme James inasema pale, "Ambaye ndani Yake ninapendezwa kukaa." Inaleta tofauti gani, "Ninayependezwa kukaa ndani Yake," ama, "Yeye ninayependezwa kukaa ndani Yake"? Mnaona? "Ninayependezwa kumkaa ndani." Hilo hapo, Mungu ndani ya mwanadamu, mbingu na nchi zikaungana. Mungu na mwanadamu wakaungana. Wakati mkuu kuliko nyakati zote, hadi wakati huo, uliowahi kuwa duniani, ama uliopata kuwako.

89 Angalia, ishara ya Nguzo ya Moto, na halafu Sauti ya ishara ikanena. Unaona? Ishara ya Nguzo, ya Sauti, ilikuwa iko pale ikiwa tayari kunena. Ile ishara ilionyesha tu ya kwamba Sauti ilikuwa tayari kunena. Mnapata hilo wazo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

90 Ile ishara inaonyesha kwamba Sauti ya Mungu iko tayari kunena, na wakati Mungu anapoonyesha ishara kama anavyofanya katika siku za mwisho. Huninii . . .

91 Hebu angalia kote. Angalia—angalia utovu wa uadilifu wa watu leo. Hiyo ni ishara ya Mungu. Unapoona watu wakiwa hivi, angalia kule wanakoelekea. Alisema, "Watazidi kuharibika zaidi na zaidi." Wao, wanafanya hivyo, unaona, hiyo—hiyo ishara ya utovu wa uadilifu. Vema.

92 Na kuna kila aina ya ishara. Ishara zilizoko juu mbinguni, maajabu ya kutisha, visahani virukavyo; Pentagon inaviangalia, hawajui ni kitu gani. Kila aina ya ishara: bahari ikivuma, mawimbi, mshangao wa wakati, dhiki miongoni mwa mataifa, mambo yote haya, matetemeko ya nchi mahali mahali, watu wakienda mbio huko na huko, maarifa yakiongezeka, mambo haya mengine yote aliyosema, misukosuko mikuu. Jinsi ambavyo Kristo angetolewa kanisani Mwake katika siku za mwisho, katika Wakati wa Laodikia, tunalo hilo. Mnaona? Mambo haya yote ni ishara za Mungu akinena.

93 Halafu ni kitu gani kitakachofanya mambo haya yajulikane? Mungu anamtuma mtu fulani jukwaani, kitu fulani jukwaani kuthibitisha jambo hilo, na kuchukua Maandiko yaliyonenwa kwa ajili ya siku hiyo na kuyadhihirisha, ndipo huo ndio utambulisho wake. Hiyo, unaona, hiyo ndiyo ishara.

94 Nguzo ya Moto, mara ninii—ishara hiyo ilipotokea pale, ilikuwa ni—hiyo ilikuwa ni ishara kwamba Sauti ilikuwa tayari kunena.

95 Nasi tunaona ishara ya wakati wa mwisho. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema,"Amina."—Mh.] Ishara ya mwisho! Ni wangapi wanaoamini jambo hilo, semeni amina. ["Amina."] Basi, Sauti hiyo iko tayari kunena! Sauti hiyo iko tayari kunena kwa sababu tunaiona ile ishara. Nguzo ya Moto ilikuwa pale kusema ya kwamba Sauti hiyo ilikuwa tayari kunena.

96 Pia, haina budi kuwa ni ishara ya Kimaandiko, haina budi kuwa ni thibitisho la Kimaandiko la Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hiyo. Jinsi utaratibu wa Mungu ulivyo mkamilifu kila wakati!

97 Sasa sikilizeni, hebu na turudi nyuma kwa muda kidogo tu hapa, wazo dogo. Katika Agano la Kale, kabla Biblia haijaandikwa, kulikuwa tu na magombo na kadhalika, haikuwa imekusanywa ikawekwa pamoja, kama Kitabu cha maandiko ya Isaya, Kitabu cha maandiko ya *fulani*, hao manabii. Sasa, kama mtu akija na jambo fulani, ya kwamba alikuwa ameota ndoto, ama alikuwa ni nabii, jambo la kwanza, walimchukua wakampeleka hekaluni, kwenye Urimu Thumimu yao.

98 Wahudumu hapa, na wengi wenu ninyi ndugu huko nje, mnajua Urimu Thumimu ilikuwa ni kitu gani. Ilikuwa ni—ilikuwa ni dereya kifuani pa Haruni. Waliitundika kwenye nguzo hekaluni. Na sasa angalia, wakati mtu huyo alipoanza kuzungumza, na, kama lolote alilosema, kama halikuwa ni kweli, hiyo Nuru haikumulika; hakuna kitu kilitukia. Lakini alilosema, kama lilikuwa ni kweli, basi mkusanyiko wa Nuru, kama upinde wa mvua, ulianza kumulika. Na hiyo iliitwa Urimu Thumimu. Ndugu wanajua jambo hilo. [Ndugu wanasema, "Amina."] Hakika. Hakika, hiyo ilikuwa ni Urimu Thumimu.

99 Ilikuwa ni kitu gani? Ishara, haidhuru ilisikika jinsi gani, ishara hiyo haina budi kutolewa pamoja na Sauti. Amina. Unaona, ishara inakuja kisha Sauti. Hapana budi iwe hivyo, la sivyo hiyo Sauti haitambuliwi. Hiyo ni kweli. Haidhuru sauti hiyo ilisema nini, ilisikika halisi jinsi gani, kama hiyo Urimu Thumimu haikuyakinisha, basi haikuwa sahihi.

100 Na ishara ya namna yoyote inayoonyeshwa leo... Ninajua ya kwamba Mungu anaweza kufanya mambo ambayo hayajaandikwa katika Biblia, bali, kwangu mimi, tunaishi katika saa tunayopaswa kuwa waangalifu sana. Urimu Thumimu leo ni Biblia ya Mungu. Hiyo inaonyesha yale yanayopaswa kutukia leo.

101 Wakati wanapowazia, "Inatupasa kujenga shirika kubwa zaidi, inatupasa tuingie katika Baraza la Ekumeni, hiyo ni ishara ya umoja." Kwangu mimi, ni ishara ya mpinga-Kristo. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema hasa. Hakika. Si ishara ya Kimaandiko; ila tu, kwa upande mwingine, inamfanya mwaminio ajue inaelekea upande gani. Urimu Thumimu ni Neno la Mungu; na yale aliyosema yangetukia katika siku za mwisho, hayo ndiyo hasa yanayopaswa kuonyeshwa. Na hiyo ni ishara ya uongo.

102 Mtu anasema, "Vema, nina Ph.D., LL.D., nilifanywa *nanii*. Mimi ni Daktari *Fulani*." Hiyo si ishara ya Biblia. "Ninajua kuhusu Hilo. Vema, mimi ndiye kiongozi wa *Ninii*. Mimi ni mkuu wa wilaya. Mimi ni—mimi ni askofu. Mimi ni..." Sijali wewe ni nani.

103 Kuna ishara moja tu tunayoiangalia, na hiyo ni Neno la Mungu lililothibitishwa, wakati ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ndiyo Sauti ya ishara, Neno la Mungu kwanza. Wakati Urimu Thumimu iliponena, wao walisema, "Hiyo ni kweli." Wakati hizo Nuru zilipomulika, ishara ilikuwapo pale, Sauti hiyo ilikuwa ni ya kweli. Angalia jinsi ambavyo-jinsi ambavyo watu wamelibatilisha hilo leo, kwa mapokeo yao!

104 Yesu Kristo alisema, katika agizo Lake la mwisho kwa kanisa Lake, katika Marko 16, baada ya kufufuka Kwake; Yeye alisema, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokolewa; asiyeamini atahukumiwa. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Kama hilo halimuliki kwenye Urimu Thumimu ya maisha yako, kuna kasoro fulani. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; kama wakishika nyoka, ama kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Na mtu mwenye elimu nzuri, kufikia kiwango cha juu sana, anakana jambo Hilo; inawezaje kuwaka kwenye Urimu Thumimu ya Mungu, wakati Yeye aliposema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio"? Neno la Mungu, lote kwa jumla, ni kweli.

105 Kwa hiyo Urimu Thumimu haina budi kumulika pamoja na ishara. Kama ishara itaninii . . . Sijali yeye anafanya nini, kama hailingani, haifanyi kulingana na Neno hilo, basi kuna kasoro fulani. Haijalishi yeye anafanya nini, kuna kasoro. Haina budi kufikia Ukweli. Hivi Yesu hakutwambia, katika Mathayo 24:24, "Roho hizo mbili zingefanana sana katika siku za mwisho, ingewapoteza walio wateule kama yamkini"?

106 Sasa vaeni kofia yenu ya kufikiri, vaeni silaha zenu za Mungu. Sikilizeni kwa dakika moja tu. Angalieni, inatupasa kuja sawasawa na jinsi alivyosema tufanye. Jinsi tu ambavyo Mungu alisema tufanye, hivyo ndivyo inavyotubidi kufanya. Yale Yesu aliyosema yatatukia, hayo ndiyo yatakayotukia. Kama Yeye alisema, "Ishara hizi . . . "

Wao wanasema, "Hilo lilikuwa ni kwa ajili ya mitume peke yao."

107 "Ulimwenguni kote, na kwa kila kiumbe!" Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni wapi Yeye alisema, "ni kwa mitume tu"? "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na, kote ulimwenguni, na kwa kila kiumbe."

108 Mtu fulani akisema, "*kule* nyuma," yeye anajaribu kuhepa jambo Hilo. Huyo si nabii. Yeye ni nabii wa dhehebu fulani, bali si nabii aliyetumwa kutoka kwa Mungu. Huenda akawa anaakisi madhehebu fulani, ama nadharia fulani, shule fulani, maadili fulani.

109 Bali ninazungumza juu ya Mungu na Neno Lake, Urimu Thumimu ya Kimaandiko, ishara ya Kimaandiko, Sauti ya Kimaandiko nyuma ya ishara.

110 Yona, yule nabii, alikuwa ishara. Ishara yake ilikuwa ni wakati alipotapika, nyangumi alipomtapika ufukoni, hiyo ilikuwa ni ishara. Watu hao walikuwa ni makafiri, kazi yao ni kuvua samaki. Nao walimwona mungu-nyangumi akija, mungu huyu wa baharini, na kumchukua nabii na kumtapika ufukoni, apate kutoa ujumbe, naye huyoo akashuka kwenda pwani. Hiyo hapo ilikuwa ishara. Sasa Sauti ilikuwa, "Tubuni la sivyo mtaangamia!" Kabla Mungu hajalipiga taifa hilo, kulirarua vipandevipande na kulizamisha chini ya bahari, Yeye alimtuma nabii akiwa na Neno Lake. Akampa ishara, ishara ya kimbinguni.

111 Kumbukeni, ishara hiyo inadumu hata leo. Yesu aliirejelea. Alisema, "Kama vile nabii Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi, kwa muda wa siku tatu mchana na usiku, ndivyo impasavyo Mwana wa Adamu. Kizazi kiovu na cha zinaa kinatafuta ishara. Nao wataipata, ishara ya ufufuo." Kama tuliwahi kuwa katika kizazi kiovu na cha zinaa, ni sasa, ambacho Yesu alisema kingekuwako. "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa atakapokuja Mwana wa Adamu."

Basi, tuko katika kizazi kiovu na cha zinaa, nao wataipata ishara ya Kristo aliyefufuka, yeye yule jana, leo, na hata milele. Yesu alisema hivyo. Hiyo ni kweli.

112 Yona alikuja, yeye alikuwa nabii. Bwana alimtuma. Alijaribu kulihepa, kama vile Musa.

113 Huwezi kuhepa swala hilo. Watu wengi wanataka kukupigapiga mgongoni, na kusema, "Njoo kwenye kundi letu. Njoo kwenye kundi letu." Hakuna cha kundi. Mungu ndiye tu uliye chini Yake. Unaona? "Njoo kwetu."

114 Naye alihepa na akaenda, akaelekea Tarshishi. Mungu akamweka ndani ya nyangumi, akamrejesha moja kwa moja. Naye akaingia mle, na hiyo ilikuwa ndiyo ishara. Nayo Sauti ya ishara hiyo, ilikuwa ni "Tubuni ama mwangamie!" Wao waliifuata hiyo Sauti kwa maana waliiamini ile ishara, wala hawakuangamia. Na hivyo ndivyo tu ilivyokuwa, kwa maana waliiamini ishara hiyo kisha wakaisikia Sauti.

115 Hiyo ndiyo njia ya pekee ambayo wafuasi wa makanisa ya siku hizi watakavyoihepa Hukumu, ni wakati watakapoamini ishara na kuisikia Sauti ya Mungu.

Sauti hiyo ilikuwa ni, "Tubuni ama mwangamie!"

116 Nuhu, yule nabii, kabla Mungu hajauangamiza ulimwengu ulioitangulia ile gharika, Nuhu alikuwa ndiye nabii. Nabii huyo alikuwa ishara. Ya nini? Kwamba hukumu ilikuwa imekaribia. Nuhu akijenga ishara yake kwao, safina aliyokuwa akijenga; akiihubiri Injili, Sauti ya Mungu ilinena, nao ulimwengu ukaangamizwa.

117 Yohana, nabii, baada ya muda wa miaka mia nne bila nabii yeyote, muda mrefu kuliko muda wowote ambapo Israeli walipata kwenda bila nabii. Mungu alikuwa akifanya nini? Kwa nini alimwacha ipite muda wa miaka mia nne? Alitaka nabii huyo aonekane kuwa mtu mu—muhimu sana kwa watu, wapate kufahamu na kutii yale mtu huyo aliyosema. Alikuwa ametabiriwa kwamba atakuja. Wao walisema, katika Malaki 3, "Tazama, ninamtuma Mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kuiandaa njia." Nao hawakuwa na nabii kwa muda wa miaka mia nne, na huyu hapa huyo nabii akaja, Yohana, jukwaani. Kutokea kwake kulikuwa ni ishara, ishara (ya nini) ya kwamba kuja kwa Masihi kulikuwa kumekaribia. Alikuwa akiwavutia Israeli usikivu.

118 Mwajua, imeahidiwa kuja tena katika siku ya mwisho, hiyo ni kweli, kuwakusanya watu tena na kuvutia usikivu wao, mioyo yao, kuirudisha kwa baba zao, hapo mwanzo. Kuchukua kanuni hizi zote hapa za imani na kadhalika, na kuziangamiza, na kurudi kwenye yale Biblia ilisema, "kuirudia Imani ya baba zao." Kuthibitisha, Mungu aliahidi kufanya.

119 Angalia sasa, kuonekana kwake kulikuwa ni ishara ya kwamba Masihi alikuwa amekaribia, miaka mia nne. Nao je! walimpokea? Hawakumwamini. Hakika, hawakumwamini. Hawakuwa na uhusiano wowote na jambo hilo, kwa maana mahubiri yake yalikuwa ni kinyume. Hawakuamini yale aliyokuwa akisema. Hata hivyo, yeye alikuwa ni ishara, kwa maana watu walijua yeye alikuwa ni nabii. Walijua jambo fulani lilikuwa liko tayari kutukia. Mnaona?

120 Kila wakati, kabla ya tukio fulani. Sasa tuliruka kurasa mbili ama tatu hapa, dakika chache zilizopita, za manabii mbalimbali. Kuwaonyesha tu, mpate kufahamu. Kabla kitu chochote hakijatukia, Mungu huja na nabii, kulithibitisha Neno Lake. Na huko kuja kwa nabii ni ishara.

121 Sasa, Yohana alikuwa ndiye ishara, kwa maana yeye alikuwa ndiye huyo nabii, ya kwamba Masihi alikuwa amekaribia. Sasa tunaona Yohana, ile ishara ya—ya ninii...ya kuja kwa Yesu. Tunajua ya kwamba wakati Mungu anapozungumza na kusema mambo haya, hayana budi kutimia. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa, ile ishara ya matayarisho, Yohana alikuwa ndiye hiyo. Alikuwa awe ishara ya matayarisho. Je! mnaamini ya kwamba alikuwa ishara ya matayarisho? ["Amina."] Vema, basi, kama alikuja wakati huo, katika ishara ya matayarisho, yeye anakuja tena katika ishara ya matayarisho.

122 Angalieni, ujumbe wake ulikuwa, na tabia yake ilikuwa, jinsi vile hasa roho aliyotiwa mafuta kwayo ilivyokuwa. Yeye alikuwa kama Eliya. Yesu alisema, "Kwa nini waandishi wanasema imempasa Eliya kuja kwanza?"

123 Akasema, "Amekwisha kuja tayari, nanyi mkamfanyia yale yaliyoandikwa. Mnaona? Vivyo hivyo imempasa Mwana wa Adamu kuteswa chini ya mikono yao, maana Maandiko yote hayana budi kutimizwa."

124 Mwangalie Yohana, angalia yale Yohana aliyofanya. Yohana alikuwa mtu maarufu sana, alitoka mahali palipo duni; vivyo hivyo na Eliya. Wote wawili walikuwa wapenda nyika. Na, kumbukeni, wote wawili waliwakemea wanawake waliojipaka nyuso rangi, wanawake waovu. Na tabia zao zilifanana; jinsi Eliya alivyokuwa hasa, ndivyo alivyokuwa Yohana. Nao wote wawili kwa namna fulani walishika njia ile ile mmoja aliyochukua, pamoja na yule mwingine.

125 Lakini Yohana alikuwa ndiye aliyemtangaza na kumtambulisha Masihi. Angalia, yeye alimtambulisha Masihi. Akiwakemea wanawake watovu wa uadilifu!

126 Angalia siku hizi, kile tunachoita manabii wa makanisa leo, na kisha wanajiita wenyewe "wa Mungu"? Baadhi ya hawa manabii wa kisasa wa Ahabu wakiwa na maskini Mayezebeli wao waliopaka nyuso zao rangi, wenye nywele

fupi, wanaovaa kaptura wakiwaongoza popote wanapotaka kwenda, kisha wanajiita madaktari, na kadhalika, "wa Biblia"? Inawezekanaje? Wao ni akina Ahabu, naam, fundisho la kanuni zao za imani, wanaogopa kuziacha, wanaogopa watatolewa kwenye madhehebu yao, ama chochote kile.

127 Hebu niwaambieni, ni karibu katika wakati huo ambapo Mungu daima huinua kitu fulani jukwaani, kuhukumu jambo hilo. Alifanya hivyo katika siku za Ahabu. Alifanya hivyo katika siku za Yohana. Aliahidi kufanya jambo hilo tena katika siku za mwisho, Naye atalifanya! Ni wakati kama huo ambapo tumeahidiwa jambo hili, kwenye wakati huo tutakapoona Malaki 4 ikitimizwa, jinsi hasa alivyosema jambo hilo; ishara ya hukumu ijayo, moto unaowaka utakaoangamiza kutokuamini kote, na wenye haki watatembea juu ya majivu ya waovu. Imeahidiwa. Imetabiriwa. Ni BWANA ASEMA HIVI. Haina budi kuwa. Sauti yake itafanya nini, wakati mtu huyu atakapojitokeza jukwaani? Itakuwa ikilifunua Neno lililoahidiwa la Yesu Kristo. Hilo ndilo jambo pekee linaloweza kuwa, kwa maana Biblia ilisema, katika Waebrania 13:8, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Kweli.

128 Yeye alisema pia, katika Luka 17:30, "Kama ilivyokuwa kaika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu, wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa." Mwana wa Adamu ametabiriwa kufunuliwa. Na itakuwa ni ufunuo wa namna gani? Itakuwa ni ufunuo wa kuishi Kwake, baada ya kusulubiwa kwa muda wa miaka elfu moja mia tisa, na amefufuka katika wafu na anaishi pamoja nasi. Yeye atafunuliwa! Kwa sababu, ni mambo yale yale waliyofanya kule Sodoma, hayana budi kurudia tena. Unaweza kulifasiri kwa njia yoyote unayopenda, lakini ndilo hilo hapo. Ni kweli tu, linajifasiri lenyewe. Neno halihitaji fasiri yoyote wakati linapojifasiri Lenyewe. Likimfunua Kristo katika ahadi ya wakati huu, hicho ndicho hasa kitakachojitokeza jukwaani.

129 Paulo, alikuwa na ishara. Hebu na tumwangalie. Je! mnaamini ya kwamba Paulo alikuwa ni nabii? Bila shaka alikuwa nabii. Sasa angalia. Paulo alijtokeza jukwaani, na akaona ishara. Je! aliona ishara ya aina gani? Nguzo ya Moto, akienda zake Dameski, akiwa ni Myahudi. Yesu alikuwa amekwisha kufa, amesulubiwa, akafufuka, akapaa Mbinguni, naye Paulo alikuwa akienda zake Dameski wakati Nuru kuu ilipompiga akaanguka. Ndipo akalia, "Bwana, U nani Wewe?"

130 Akasema, "Mimi ni Yesu." Naye aliambiwa ya kwamba alikuwa ameitwa awe chombo kilichochaguliwa, chombo kilichochaguliwa.

131 Sasa angalia, je! Paulo alikuwa na nini, ambacho hao wengine hawakuwa nacho? Alikuwa na wingi wa ufunuo wa Neno la Mungu, maana Paulo ndiye aliyetambua ya kwamba

Yesu wa Agano Jipya alikuwa Ndiye Yehova wa la Kale. Haleluya! Ningeweza kusema jambo fulani hapa. Yeye alikuwa na ufunuo wa jambo Hilo. Yeye aliliandika na kulifunua, kwa maana Mungu aliliruhusu kuongezewa kwenye Biblia. Na Neno huja tu kwa Biblia, kwa nabii. Na kwa hiyo basi Mungu alimfunulia Paulo, naye akaandika zile nyaraka, zilizovuviwa, na Mungu akaziweka katika Biblia. Loo, jamani! Akafunua ya kwamba Yeye ni Kristo wa Agano la Kale, kwa maana yeye alikutana Naye.

132 Asingeweza kuelewa jinsi ile Nguzo ya Moto ilivyokuwa. Hiyo ndiyo iliyowaongoza watu wake toka Misri. Hiyo ndiyo iliyokuwa pamoja na Waebrania kote kote katika wakati huo. Na, ndiye Huyu hapa, yeye alimwona. Akasema, “Bwana, unataka nifanye nini?”

Akasema, “Mimi ni Yesu.”

133 Aliona ya kwamba Huyu aliyekuwa amewaongoza watu wake, ambaye alimfahamu wakati wote, ambaye Musa alikutana naye, yule “MIMI NIKO,” aliyepo daima, yeye yule jana, leo, na hata milele, alidhihirishwa katika mwili. Ulikuwa ni ufunuo wake. Alikuwa nao zaidi ya hao wengine wote. Alikuwa . . . naye alikuwa nao kiasi kikubwa sana mpaka . . . asije akajitukuza juu ya wingi wa ufunuo aliokuwa amepewa. Loo, jamani!

134 Yeye alifanya nini? Ufunuo wake wakati huo ulikuwa ndio unabii wa siku hii. Ulikuwa ni Sauti iliyotoka, ikaandikwa katika Biblia, ipate kuthibitishwa tena leo. Haleluya! Ndiyo Sauti inayothibitishwa tena, yale aliyoandika, kwa maana yeye alikuwa ni nabii wa Mungu, akifunua. Hiyo ishara ilikuwa ikizungumza jambo fulani.

135 Na tunaona sasa ya kwamba, Yesu, wakati alipojitokeza jukwaani, angalia, Yeye alikuwa ndiye Neno lililotabiriwa. Alikuwa na huduma ya kutimiza. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakika, Yeye alikuwa na huduma, angalia, ya kutimizwa, yale yaliyoandikwa juu Yake. Kasema ya kwamba, hivi majuzi usiku kama nilivyozungumza, juu ya Kleopa na hao wengine, “Enyi msiofahamu, na wenye mioyo mizito ya kuamini Neno la Mungu. Je! hamjui inampasa Kristo kupata mateso haya? Je! hivi manabii wote hawakunena ya kwamba Yeye ingempasa kufanya jambo hili, na kisha kuingia katika utukufu Wake?” Inambidi kutimiza kila kitu kilichomleta. Alikuja kuponya, lipate kutimizwa. Alifanya *hivi*, lipate kutimizwa. Kila kitu alichofanya kilikuwa ni cha kutimiza, kwa maana ilimpasa kuwa Sauti ya Maandiko hayo. Lakini kabla hajafanya jambo hilo, Yeye alitoka kwenda na huduma ya uponyaji, akawaponya wagonjwa. Kila mtu alitaka kuona ile ishara. Hakika, waliamini ule uponyaji, bali ile Sauti ilibadilisha mambo.

Siku moja, wakati Yeye aliposema, "Mimi na Baba ni mmoja."

136 Hilo, hilo lilikuwa limezidi mno kwao. "Unajifanya Mwenyewe kuwa Mungu, ukiwa u mwanadamu." Wakati ile—ile ishara, wao waliiamini, bali wakati waliposikia Sauti nyuma yake, huduma fulani iliyoifuata ishara hiyo, hawakulipata. Hapo ndipo shida ilipoanza.

137 Kumbukeni, Yeye aliwachagua kumi na wawili. Alisema, Yeye "aliwachagua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Alisema, "Nimewachagua kumi na wawili, na mmoja wao ni ibilisi." Ilimbidi Paulo kupachukua mahali hapo, kuwa aliyechaguliwa.

138 Na tazama, na wakati alipofanya hivyo, siku moja alianza kuzungumza na watu, na akasema, "Msipoila nyama ya Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hamna Uhai." Madaktari wangesema nini juu ya hayo? Sasa, Yeye kamwe hakuelezea jambo hilo. Kamwe hakusema ninii yoyote . . .

139 Yeye alikuja tu kwa ajili ya idadi fulani ya watu. Wale aliokuwa ametangulia kuwajua, Alikuja. Yeye, Yeye akasema, "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba, watalifahamu, watakuja. Unaona? Unaona, watakuja. Watalifahamu Hilo, wao ambao Baba amenipa Mimi, ambao majina yao yako kwenye Kitabu cha Uzima." Yeye alikuja kuwakomboa.

140 Sasa tunaona ya kwamba, katika hiyo—katika ile saa kuu, Yeye alisema, "Msipoila nyama ya Mwana wa Adamu, kuinywa Damu Yake."

141 Ungeweza kuwazia kile watu walichofikiria? "Je! mtu yule amerukwa na akili? Hivi Yeye anataka sisi sote tuwe wala watu? Na sasa labda atatoka aende mahali fulani na kujiua, nasi tunapaswa kuila nyama Yake na kuinywa Damu Yake?" Unaona, wao kamwe hawakulifahamu.

142 Yeye alimwambia Nikodemo, kasema, "Kama nikikwambia mambo ya duniani, wala huyafahamu, utafahamuje mambo ya Mbinguni, kama nikikwambia." Unaona? Kwa hiyo, tunaona ya kwamba hawakufahamu jambo hilo. Kwa hiyo, kusanyiko likapungua.

143 Kwa hiyo basi akasema, tena, "Mtakapomwona Mwana wa Adamu akipaa juu mahali alikotoka."

144 Ndipo wale wahudumu sabini, shirika hilo lote, likasema, "Mtu huyu ana shida gani? Ati Mwana wa Adamu akipaa juu? Na hapa sisi tunakula pamoja Naye, tunalala pamoja Naye, tunavua samaki pamoja Naye, huko nje milimani pamoja Naye, tulilala nyikani pamoja Naye, kwenye fuo za vijito vidogo pamoja Naye, halafu basi na kupanda juu; tumeona kitanda kidogo alimopembezewa, tukazungumza na mama Yake, tukamjua

Yusufu, alidhaniwa kuwa ni baba Yake. Tunajua mambo haya yote. Na ndipo akasema, ‘Mwana wa Adamu anapaa juu mahali alikotoka.’ Loo, hilo linawezekanaje?” Unaona? Lakini Yeye alikuwa ndiye lile Neno. Walikosa kuona ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Neno.

145 Kama nilivyonukuu hivi majuzi, moja ya Maandiko mazuri sana, ya kwamba wakati Yesu, akiwa na umri wa miaka kumi na miwili, wakati walipomwacha kwenye Karamu ya Pentekoste, walikuwa wameondoka kwa muda wa siku tatu wala wasingeweza kumwona. Walirudi. Mariamu alikuwa ameshuhudia dhahiri kabisa kwamba, kwamba “Roho Mtakatifu alimtia uvuli” na ndipo akamzaa Mtoto huyo. Lakini wakati alipomkuta hekaluni, akibishana na hao wanasheria, yeye alisema nini? Alisema, “Baba yako na mimi tumekutafuta kwa huzuni.” Alifanya nini? Alikana ushuhuda wake mwenyewe, kumwita Yusufu baba Yake. Sasa, kama yeye ni mama wa Mungu, na hilo je? Unaona?

146 Angalia, Neno daima ni lenye kusahihisha. Maskini Mvulana huyo mwenye umri wa miaka kumi na miwili, kamwe hakuwa ameenda shuleni hata siku moja, tujuavyo sisi, ni Mtoto tu. Yeye hakujua kamwe alitamka jambo hilo, labda, bali angalia yale aliyosema, “Hamjui ya kuwa imenipasa kuwa kwenye shughuli za Baba Yangu?” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

147 Naye Ndiye Neno leo! Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. “Hamjui?” Kama angalikuwa kwenye shughuli za Yusufu, angalikuwa akifanya kazi ya seremala. Lakini alikuwa akifanya kazi za Baba, kazi za Baba wa Mbinguni. Alikuwa huko nje akiyalipua hayo madhehebu waliyokuwa nayo kule, na yote yaliyohangaisha. Alikuwa akiyararua vipandevipande. Nao walishangaa sana, Mvulana mdogo wa jinsi hiyo, aliyejua hayo. Ilikuwa ni Mungu akinena kupitia Kwake, kwa maana Yeye alikuwa ni Neno la siku hiyo. Angalia jinsi hilo lilivyo kamilifu. Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

148 Ufunuo Wake, tunaona, ni ule ule. Yeye—Yeye alianza kuponya, na, wakati akifanya jambo hilo, kila kitu kilikuwa ni shwari. Lakini basi wakati alipoanza kuninii, ni ile Sauti, ikaanza kunena, “Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu.”

149 Vema, wao, kusanyiko hilo, liliondoka. “Loo, mtu huyo, hatutaki kumsikiliza tena. Mtu huyo amerukwa na akili.”

150 Walisahau yote aliyokuwa amefanya, yale madhihirisho. Hawakusoma Biblia, wapate kuona saa waliyokuwa wakiishi. Hakika, Yeye alikuwa ni mtu wa kipekee. Mungu hufanya jambo hilo jinsi hiyo. Wanasema mambo ya kipekee.

151 Ni kwa nini—ni kwa nini Mikaya asingeweza kukubaliana na manabii hao wengine wa Israeli kule, mbele ya Yehoshafati na hao wengine? Unaona? Ni kwa nini asingekubaliana nao? Yeye alikuwa na Neno la Bwana, ilimbidi aseme. Alisema, “Nitasema

tu yale Mungu aliyosema." Nao walikuwa na mamlaka ya Kimaandiko kuonyesha ya kwamba walikuwa sahihi, bali si Maandiko yote. Yesu alisema, "Pia imeandikwa." Unaona? Wao hawakufahamu.

152 Sasa angalia tunapofunga sasa. Tuna—tunachelewa. Naam, samahani nimeenda kwa kirefu sana, nami nitaharakisha upesi sana sasa kwa ajili ya mstari wa maombi. Ni maneno machache tu zaidi ninayotaka kusema hapa.

153 Angalia, nabii alikuja, na anapokuja, inaonyesha ishara, na halafu kuna Sauti fulani katika ishara hiyo, ambayo hunena, Sauti ambayo inanena, Sauti ya Kimaandiko ambayo inapaswa kuwa ni kulingana na Biblia, ikiakisi Neno kwa wakati huo. Daima imekuwa hivyo, daima itakuwa hivyo, kwa kuwa Mungu hawezi kubadilika.

154 Sasa angalia huduma ya kwanza ya Yesu, loo, hao wote, kila mtu, alimtaka kanisani mwao, "Loo, jamani, Yeye ni Mtu mkuu!" Hakika, Yeye alikwenda kwenye masinagogi yote, akasoma magombo na kuketi chini. Kila mtu, "Rabi kijana!"

155 Lakini siku moja alianza kuwazungumzia kwa namna nyingine, ile Sauti ya ishara ilianza kunena. Na wakati Sauti hiyo ya ishara ilipoanza kunena, hakuna mtu aliyemtaka. Mmoja wao alisema, "Mtu huyu ana kichaa. Ni mla watu, akijaribu kutufanya sisi sote tuwe wala watu." Unaona? Yeye kamwe hakuelezea jambo hilo. Aliwaacha waende zao.

156 Wengine waliofuata, tunaona ya kwamba wale sabini, lile shirika la wahudumu aliokuwa pamoja nao, walipokuja, "Vema, Mtu huyu anawezaje kupaa juu? Vipi? Kwani Yeye ni nani? Mbona, hapa anajifanya kuwa sawa na Mungu. Hilo ni neno gumu." Nao wakaondoka wakamwacha.

157 Ndipo akawageukia wale wanafunzi, na kusema, "Je! mnataka kwenda, pia?" Unaona? Wasingeweza kwenda. Walikuwa wameona jambo fulani. Walijua Maandiko na walijua jambo hilo lilikuwa ndilo lenyewe. Hawakuweza kuelezea yale aliyokuwa akinena habari zake, bali waliyaamini hata hivyo. Kamwe hawakuuliza maswali; halikuwasumbua. Waliamini kwa sababu ilikuwa ni thibitisho la Maandiko. "Je! mnaamini jambo Hilo?"

158 Petro alisema, "Bwana, tungekwenda wapi? Wewe peke yako una Maneno ya Uzima wa Milele." Waliona jambo hilo. Walijua jambo hilo, Yeye, kwamba Yeye-kwamba Yeye alikuwa ni nani, na hayo ndiyo aliyopaswa kufanya. "Haidhuru, hatuwezi kulielezea." Unaona, walikuwa wamechaguliwa kuupata Uzima, kabla ya kuweka misingi ya ulimwengu. Wakati Nuru hiyo ilipoigusa, walijua jambo hilo. Hakuna kitu kingaliwaondoa kwake, hata iweje. Ilionekana kana kwamba Mafarisayo walikuwa wamembana, upande mmoja na mwingine, halikuwasumbua hao wanafunzi. Walisonga mbele

moja kwa moja, hata hivyo, kwa kuwa waliamini jambo hilo. Sauti Yake ilinena wakati huo.

159 Sasa huenda nikasema jambo hili. Sauti Yake itazungumza siku moja, ishara itakuja, nayo itafanya nini? Ishara ya Laodikia haina budi kuwa jinsi ilivyokuwa wakati huo. Kutakuwa na Sauti itakayotuzungumzia katika siku ya mwisho. Kumbukeni, ishara ya Laodikia! Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele; na wakati alipotolewa nje ya kanisa pale. Katika wakati wa Laodikia, tunaona, Yeye anatolewa nje tena, yuko nje.

160 Angalia, ile Sauti, "Kama Mtu yeyote atashirikiana, kama mtu yeyote ataniruhusu niingie ndani, nitakuja na kula pamoja nao, nao pamoja na Mimi. Nitaingia na—na nita—nitakuwa ndani yao." Akisimama nje ya utaratibu wa wakati wa kanisa, akibisha, akijaribu kuingia. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara saba—Mh.] "Mtu yeyote akifungua mlango na kushirikiana na Mimi kidogo, nitaingia na kula pamoja nao. Nitajitambulisha kwao. Kama tu ningaliweza kuingia, kama nilivyofanya kwenye barabara ya kwenda Emau usiku ule, huko Emau. Kama ninaweza tu kuingia, nitajitambulisha Mwenyewe kwao." Sasa, Biblia ilisema ya kwamba hivyo ndivyo ingekuwa, na hivyo ndivyo ilivyo.

161 Kristo, "Kula, kujifunua Mwenyewe kwao, nitafunua ya kwamba ni Mimi yeye yule jana, leo, na hata milele. Mwana wa Adamu atafunuliwa katika siku hiyo, wakati ukanisa-kanisa wote na chochote kile vimekuwa Sodoma na mambo mengine namna hiyo. Nitakuwa nje, bali nitakuwa nikibisha, nikijaribu kuingia."

162 Sasa, tena, laiti ungeweza kuamini dhi—dhihirisho la kweli la wakati huu tunaoishi! Sitapata wakati wa kuendelea kupitia katika jambo hili. Lakini kama hamwezi kulipata, na mnaweza kuona sasa, dhihirisho la kweli; ya kwamba Mungu huonyesha ishara, na ishara hiyo ina Sauti ya Kimaandiko. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Na tuombe.

163 Bwana Yesu, neno moja tu kutoka Kwako sasa, la thibitisho, ya kwamba ni kweli. Sasa, Baba wa Mbinguni, tunatambua kile kingekuwa ndicho mwisho wetu kama tukikutwa sisi ni shahidi Wako wa uongo. Ningeenda wapi, Bwana, ni nini kingenipata? Mwisho wangu ungekuwa wapi, kama nikipatikana kuwa shahidi wa uongo, ama nimejenga nyumba juu ya mabua makavu ama mchanga udidimiao? Mungu, tusaidie, waaminio halisi, kama itatubidi kusimama peke yetu, kusimama juu ya Neno. Tunaona ishara Yako, Bwana. Tunaona ya kwamba jambo fulani linakaribia kutukia. Tunajua ya kwamba wakati wa mwisho umewadia. Tunajua imeahidiwa kwetu, sasa jalia tusishindwe kuona jambo hilo. Njoo, Bwana Yesu. Wewe ni yeye yule. Wewe ni Yesu, usiku wa leo. Wakati unapoweza kumpata mtu

wa kukukaribisha tu ndani, ili kwamba uweze kuingia, basi utajitambulisha kwao. Tujalie, ninaomba usiku wa leo, kwa Jina la Yesu. Amina.

164 Nimechelewa kidogo tu, wapendwa. Nitachukua kama dakika kumi ama kumi na tano, tulizo nazo. Nitawaita wachache, mstari wa maombi. Sikuangalia saa yangu kamwe.

165 Nina saa niliyopata huko Uswisi, nilipewa. Ninaitia ufunguo na inapiga kengele, lakini kengele hiyo ni . . . Sinayo wakati huu. Nilisahau kuileta. Sasa, inanitatiza mara nyingine. Nilihubiri kwa muda mrefu mno. Samahani. Labda nitalipia deni jambo hilo, labda kesho usiku.

166 Kadi za maombi, hiyo ilikuwa ni kitu gani, ilikuwa ni namba ngapi? Alisambaza kadi zipi za maombi? En-he? E, ati moja mpaka mia moja? Tulianza wapi wakati uliopita, kuna mtu anayekumbuka? Moja, kuanzia moja, halafu mpaka hamsini; ama ishirini na tano ama mahali fulani, ilikuwa hamsini wakati huo. Hebu na tuite kutoka sabini na tano basi, usiku wa leo. Tuliita kutoka moja, ishirini na tano, na hamsini, sasa hebu tuite kutoka sabini na tano.

167 E, sabini na tano, ni nani ana kadi hiyo ya maombi, inua mkono wako. Kadi ya maombi E, sabini na tano, inua mkono wako. Angalieni kila mahali kwenye kadi zenu. Mnataka kusema haipo hapa? Basi tuanzie mahali fulani . . . Loo, samahani. Vema, E, sabini na tano, mama. Vema. Njoo hapa, mama, papa hapa, sabini na tano. Sabini na sita, sabini na saba, sabini na nane, sabini na tisa, themanini, hebu hao watano wasimame. Moja, mbili, tatu, nne, tunakosa mtu mmoja. Moja, mbili, tatu, nne, *hii* hapa tano. Vema. Vema. Themanini mpaka themanini na tano, wasimame, katika E, themanini mpaka themanini na tano.

168 Sasa kumbukeni, kila mmoja wenu aliye na hizo kadi ataitwa. Msifadhaike hata kidogo. Tutaifikia. Themanini mpaka themanini na tano, vema. Themanini na tano hadi tisini. Mbili, tatu, nne, tano. E, themanini na tano mpaka tisini. Themanini na tano, themanini na sita, themanini na saba, themanini na nane, themanini na tisa, tisini. Tisini mpaka mia moja, katika E, hebu wasimame. Njoni upande *huu*.

169 Ndugu Roy, nisaidie kuwahesabu, angalia kama wako hapo, hebu kidogo, wakati nikininii . . .

170 Sasa angalieni, wengine wenu hapa hamna kadi za maombi, hata hivyo ninyi ni wagonjwa. Mnataka nguvu za Mungu za uponyaji, baraka za Mungu za uponyaji. Kama hivyo ndivyo ilivyo, inua mkono wako, useme, "Ninajua Mungu anaweza kuniponya."

171 Vema, tafadhali, shuka uende pale, Ndugu Roy, na umsaidie upesi sana, tafadhali, maana tumechelewa. Shuka uende ukawasaidie, tafadhali, upesi sana. Na . . .

172 [Ndugu fulani anamwambia Ndugu Branham, "Ingefaa useme hayo katika Kihispaniola."—Mh.] Naam. Anataka lisemwe kwa Kihispaniola. [Mtu fulani anasema, katika Kihispaniola, "Del número noventa a cien, noventaiuno, noventaidos, noventaitres, noventaicuatro, noventaicinco, noventaiseis, hasta cien."] Naam, yeye alisema hilo, unaona, huyu hapa mmoja anakuja sasa ambaye asingekuja. Unaona?

173 Mngeshangaa jinsi ilivyo katika nchi za ng'ambo, labda kama wakati mmoja huko Afrika. Nilikuwa na wakalimani kumi na watano wamesimama pale, mbele ya watu kama elfu mia mbili. Nami ningesema, "Yesu Kristo, Mwana wa Mungu," na lingeendelea huko chini ya mstari *huu*, na huko chini ya mstari *ule*, kwa kila kabila. Kisha ungerudi na ingekubidi kuwazia yale uliyokuwa ukisema. Na ni tofauti tu . . . Loo, jamani. Lakini nimeona wenyeji elfu thelathini wanaovaa blanketi wakimpa Yesu Kristo moyo wao, wakivivunja vinyago vyao sakafuni, kama dhoruba ya vumbi. Vema.

174 [Mtu fulani anasema sasa, katika Kihispaniola, "Mejor del número setentaicinco en adelante, del setentaicinco a cien."—Mh.] Vema. Je! kuna mtu anayekosekana hapo, ama chochote kile kingine? Naam, inalihakikisha jambo hilo. Hilo ni sawa, ndugu. Ati, hivi ulipata kuninii . . . Je! unamjua Ndugu Espinoza? ["La, simjui."] Naam, yeye anatoka huku.

175 Kuna mtu yeyote anamjua Ndugu Espinoza, yule mhudu- . . . Ndiye aliyekuwa pamoja nami huko kwenye Jiji la Mexico, wakati maskini yule mtoto mchanga alipofufuliwa katika wafu wakati ule. Ni—nilifikiri tu yeye . . . kidogo. Mmeisikia hadithi yake, bila shaka. Ilikuwa kwenye gazeti la Sauti ya Wafanyabiashara na kadhalika hapa. Nilikuwa tu . . . Ninataka kushuka kwenda kule chini tena wakati mmoja. Jamani, jinsi watu hao walivyo wanyenyekevu sana, na waliamini kweli. Walikuwa . . . Unaona, kanisa kule daima linaahidi jambo fulani, kamwe hawalifikii. Lakini hapa katika ahadi ya Biblia, tuko tunaifuatilia; ni ya kwetu, tu—tu—tunaiona, na hilo linaifanya kuwa halisi. Vema.

176 Sasa, sasa kila mmoja wenu anisikilize kwa makini sana, kwa kama dakika kumi.

177 Labda nimeita wengi kupita kiasi. Sijui, hu—huenda nilifanya kosa. Vema, kwa namna fulani waliwageuza pale. Vema, waacheni tu waende moja kwa moja waingie mstarini, Billy, jinsi tu wao—wako hivyo. Na hebu sisi tuninii tu—hebu tuanze tu, kuanza mstari wa maombi. Njoni. Wapatieni kiti ili waweze kuketi chini hapa, Ndugu Roy, ama yeyote yule. Ukumbini kule kuna nafasi. Ninataka kuona hao watu wakiangalia.

178 Unaona, kuna jambo moja usiloweza kufanya, huwezi kuwa na usumbufu. Roho Mtakatifu ni mwoga. Ni wangapi wanaojua

jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Unaona, hamna budi kuwa watiifu wakati huo.

179 Ni wangapi wamekuwa katika mkutano na kuona vitu vikitoka kwa mtu mmoja na kwenda kwa mwingine? Hakika, mmeona. Unawaona wakirukwa na akili, na kuingia wazimu; viti vinaruka na kuzungukazunguka jengoni, na pepo wakatolewa. Wengine wao wamelemaa, na ilibidi wabebwe watolewe jengoni; wangali wamelemaa, pia. Wengine wao walikufa papo hapo, mahali pale pale walipokuwa wamesimama; na wakaanguka wakafa, moja kwa moja tu mbele zetu. Unaona, hatuigizi kanisa. Ni Roho Mtakatifu. Hamna budi kuamini.

180 Mtu fulani alisimama wakati mmoja, akijaribu kunifanyia kupumbaa akili, kule Canada. Ni upi ule ulio ng'ambo ya Detroit, ni mji upi ulioko kule juu? [Mtu fulani anasema, "Edmonton."—Mh.] La, ng'ambo ya pili kutoka Detroit. ["Windsor."] Windsor. Naam, alikuja kule. Walikuwa wamemkodisha kwenda kuwapumbaza watu akili, kwa ajili ya jeshi. Mnajua, kuwafanya wabweke kama mbwa, na mambo kama hayo. Na jamaa huyo ameketi pale; ninaendelea kuhisi roho wa ajabu, na niliiona hiyo. Ndipo Roho Mtakatifu akasema mwite, kasema, "Ewe Mwana wa ibilisi, kwa nini akaweka hicho moyoni mwako kuja hapa? Kwa kuwa umefanya jambo hilo, watakubeba wakutoe hapa." Yeye angali amepooza. Hilo limekuwa ni kama miaka kumi na miwili iliyopita. Walimbeba wakamtoa nje. Naam.

181 Mungu angali Mungu. Jambo hilo ni kweli, unaona. Ni yeye yule! Habadiliki kamwe. Kama tu tunaweza kuamini, hilo tu ndilo linalotupasa kufanya ni kuwa na imani. Sasa angalieni upande huu na mwamini.

182 Sasa, kama Roho Mtakatifu akipenda, usiku wa leo, sijui kama atapenda. Lakini kama atakuja sasa, ni ishara ya aina gani tunayotarajia leo? Kufufuka kwa Kristo, thibitisho la kwamba Yesu yuko hai miongoni mwetu. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kila mtu anakumbuka? Hivi Biblia . . .

183 Sasa je! tuna ishara ya Sodoma, ulimwenguni leo? Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Tuna ishara ya Nuhu, ulimwenguni leo. Hiyo ni kweli? ["Amina."] Je! tuna mambo haya mengine yote? Sasa ni kitu gani Yeye alisema kingetukia wakati huo? "Mwana wa Adamu angefunuliwa katika siku hiyo." Hiyo ni kweli? *Kufunuliwa* ni nini? "Ni kutambulishwa." Kitu chochote kilichotambulishwa kimefunuliwa. "Mwana wa Adamu atatambulishwa katika siku hiyo." Vema, kama ni Yeye yule jana, leo na hata milele, je! Yeye si angefanya jambo lile lile kujitambulisha? Ni wangapi wanaoamini jambo hilo? ["Amina."] Vema.

184 Sasa je! mna ninii zenu . . . kila mtu yuko sawasawa hapo mstarini sasa? Sasa, wapendwa, sijui kama tutawafikia wote.

185 Ninawataka ninyi nyote kwa muda wote mwangalie kwa makini sana, na muwe na kicho, mwombe, mwamini. Sasa, tafadhalini, mnaona, hasa sana kama jambo fulani likitukia kutoka kwangu, mtu yeyote asiruke na kwenda kuninii . . . Mnaona? Naam.

186 Yapata miezi miwili iliyopita, kanisani mwangu, Jumapili moja asubuhi, kulikuwa na jambo fulani, Shetani alikuwa akifanya jambo fulani kuvutia usikivu wa watu. Kulikuwa na mwanamume mmoja Mwingereza pale, jina lake Way. Yeye anaishi kwenye ninii yangu . . . Mkitaka anwani yake, ama tunaweza kuwaambia mwandike. Yeye hutuma kanda za mikutano kutoka ng'ambo. Na mtu huyu alichukia yale niliyosema, kimoyomoyo. Nami nikaangalia chini, nikaona hiyo roho mbaya sana juu yake.

187 Nilikuwa naye katika mahojiano ya faraghani, nikamwambia. Nikasema, "Bw. Way, una ugonjwa wa moyo." Hata alichukia hilo. Nikasema, "Kwa nini ukaja kwangu, basi?" Kwa hiyo yapata mwezi mmoja baada ya jambo hilo, alienda kwa daktari, naye daktari akasema alikuwa na ugonjwa mbaya sana wa moyo.

188 Kwa hiyo alikuja mkutanoni asubuhi hiyo, na jambo fulani lilisemwa; Mwingereza mkali sana, unajua, alichukizwa na jambo hilo. Mke wake, mwanamke mzuri sana Mnorwe, muuguzi, naye alikuwa ameketi pale pamoja naye. Ndipo nikasema jambo fulani, naye akachukizwa nalo upesi sana, unajua. Na wakati alipofanya jambo hilo . . . Alikuwa amesimama kwa miguu yake, na watu walikuwa wakiimba. Na wakati yeye alipofanya jambo hilo, kichwa chake kikapinda nyuma, macho yake yakabingirika moja kwa moja nyuma, uso wake ukageuka kuwa mwekundu sana, kama lile dawati pale. Akaanguka akafa, sakafuni.

189 Vema, sasa, kanisa likaendelea tu, watu wakipiga kelele. Nami nikasema, "Ketini. Mmefunzwa vizuri zaidi kuliko hivyo. Mmefunzwa vizuri zaidi kuliko hivyo."

190 Na kwa hiyo mke wake akainama chini, alikuwa akiupima moyo wake. Alikuwa ameaga dunia. Akaanza kupiga mayowe. Nikasema, "Dada Way, hebu kidogo, mpaka nitakapoweza kutoka mimbarani hapa. Hatujui kile Baba . . . "

191 Nami huyoo nikashuka nikaenda pale, alikuwa amekauka tu. Macho yake, hakukuwa na rangi machoni mwake, yalikuwa yemetokeza namna *hiyo*, nyuma. Nisingeweza kuhisi moyo zaidi nilivyoweza kuhisi katika *kile*. [Ndugu Branham anapigapiga kitu fulani kigumu—Mh.]

Huyo dada akasema, "Loo!" Akaanza kupiga mayowe kwa nguvu, akaanza . . .

192 Nikasema, "Sasa hatujui kile Baba wa Mbinguni atakachofanya." Nami nikasema, "Labda Yeye alifanya jambo hili kwa kusudi fulani." Nikasema, "Ndugu Way alikuwa akichukia."

193 Kasema, "Alininong'onezea, ya kwamba alikuwa akichukia yale uliyosema."

Nami nikasema "Haikumpasa kufanya hivyo."

194 Nikasema, "Baba wa Mbinguni, msamehe Ndugu Way kwa kosa lake, nami ninaita roho yake irudi."

195 Akatamka, "Ndugu Branham," naye huyo hapo hai tena, akisimama miongoni mwetu. Mnaona? Mnaona? Msininii . . .

196 Kama kitu chochote kikiondoka, nyamazeni tu, nyamazeni. Nimeona jambo hilo likitukia mara nyingi sana. Lakini kama kanisa likiingiwa na wasiwasi, basi, mnaona, mnamhuzunisha Roho Mtakatifu. Sasa kama ukitaka kumsifu Mungu kwa ajili ya jambo fulani, hilo ni sawa. Lakini wakati kila mtu anaruka na kuangalia *hili*, *lile*, na watu wakisimama, na kutembea huku na huko na kuzungumziana, ni machafuko tu. Wewe . . . Yesu hata asingeweza kuwaponya watu namna hiyo, Yeye Mwenyewe. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Wakati alipokuwa hapa, Yeye aliwaongoza akawatoa nje ya mji namna hiyo, na kuweka mikono Yake juu yao kisha akawaombea.

197 Sasa, sasa, mama huyu anayesimama hapa, yeye ni mwanamke mwenye umri mdogo kuliko wangu. Anaonekana ni mwenye afya na mwenye nguvu. Sijui. Sasa, mnaona, kanisa la jana, ni wakati wa Mungu wa kuthibitisha; mwekee mikono na umwombee, mwache aondoke, uone kama alikuwa na imani ya kuponywa. Hivyo ndivyo Mungu alivyofanya jambo hilo. Lakini Yeye aliahidi jambo lingine sasa, unaona, Neno, ahadi kwa ajili ya siku hii. Nina hakika mnafahamu ninalomaanisha.

198 Sasa ninapata badilisho hapa mahali fulani. Kwa hiyo . . . [Ndugu Branham anarekebisha maikrofoni—Mh.] Naam, nafikiri hii ni bora zaidi sasa.

199 Sasa, kama mama huyu . . . Simjui mimi, bali Roho Mtakatifu anamjua.

200 Sasa hii hapa picha ya Biblia hasa, kimandhari. Kama ulipata kuwa huko kamwe, kama tu ilivyo sasa, kile kisima kingali kipo, na mizabibu imekua juu yake. Yesu alikutana na mwanamke fulani na akamwambia shida yake ilikuwa ni nini, naye akajua hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya wakati huo, ya kwamba Masihi alikuwa yupo hapo. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yule mwanamke alijua. Alilijua jambo hilo.

201 Vema, kama ni yeye yule leo, Naye aliahidi kujifunua Mwenyewe vivyo hivyo, basi itabidi iwe ni ishara Yake tena.

202 Sasa ninatumaini kila mtu anafahamu ya kwamba simaanishi ya kwamba huyo ni mimi, wala simaanishi ya

kwamba ni ndugu zangu hapa, ama mtu fulani huko nje. Ninamaanisha ni Yesu, mnaona, Kristo, si . . . mtiwa mafuta, mnaona. Mnaona, Yeye alikufa apate kuifanya huduma Yake iendelezwe na Kanisa Lake ambalo linatambua Neno Lake. Hilo halimaanishi hilo lilileta—lilileta tofauti yoyote kwangu kuliko yeyote wa watu hawa hapa, hata kidogo, ama mmoja aliyeko huko nje. Sisi sote ni wenye dhambi waliookolewa kwa neema.

203 Bali ni ahadi Yake! Yeye aliahidi kufanya jambo hilo. Na hiyo ndiyo sababu ninasimama hapa sasa, kwa sababu Yeye aliahidi jambo hilo, Naye alisema, "Nenda ukalifanye." Kwa hiyo, hilo, hakuna hofu basi.

Sasa, mama, ninataka uniangalie, kidogo tu.

204 Kufundisha na kuhubiri. Kwa kawaida mikutano yangu ilipofanikiwa sana, katika utambuzi, na kadhalika, ni wakati meneja alikuwa akihubiri, Bw. Baxter na hao wengine wangehubiri kwa muda kidogo. Na haikunibidi kufanya jambo lolote ila kwenda jukwaani, nikatoka moja kwa moja chumbani kutoka mahali fulani, nikiomba, nikatoka nikaenda moja kwa moja. Walikuwa tayari wameufanyiza mstari wa maombi. Niliingia tu moja kwa moja, unaona. Lakini, sasa, inakubidi kujigeuza tena.

205 Kuhubiri ni kipawa, kuhubiri kulikovuviwa—kulikovuviwa. Unaona? Na kipawa hicho, wengine ni mitume, wengine ni manabii, wengine ni walimu, wengine ni wachungaji, wengine ni wainjilisti. Hivyo ndivyo vipawa vilivyoko Kanisani. Mnaona? Lakini inawezekana ya kwamba tungeweza kuwa na zaidi ya kimoja, kama vile Paulo, ama yeyote wa hao. Sasa, mradi—mradi tu kuna mitume, inabidi kuwe na nabii. Mradi tu kuna nabii, inabidi kuwe na mwi—mwinjilisti. Ni kwa nini wahudumu husema, "Kuna mchungaji na mwinjilisti, bali hakuna nabii"? Unaona, huko ni kuchagua unalotaka, kulifanya liseme jambo fulani ambalo halisemi. Lakini Mungu Ndiye anayejifasiria Neno Lake. Yeye husema kama ni kweli ama si kweli.

206 Sasa kama Roho Mtakatifu atanifunulia jambo fulani ambalo umefanya, ama wewe ni nani, ama lolote lile. Ninamaanisha, sijui, unaona. Ni kama ndoto tu; unaona jambo fulani, linarudi tu nyuma. Na lolote nisemalo . . .

207 Ninachoona, ninasema. Unaona? Na basi hiyo ni ishara, unaona, na kuna Sauti ya hiyo ishara. Ishara itafanya jambo hilo; Sauti ni kile inachosema. Basi kama hiyo ni kweli, na hayo yote ni Kweli, basi yale ninayohubiri hapa juu ya Neno hili hayana budi kuwa ni kweli, maana huo ndio utambulisho wa wito. Sasa hivi hilo halikuthibitishwa na Biblia usiku wa leo? Sasa je! wasikilizaji mnaamini hilo kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Sasa hili linapaswa kulitatua.

208 Sasa, simjui mwanamke huyu. Huu hapa mkono wangu umeinuliwa, na hili hapa Neno la Mungu, na hawa hapa wahudumu wameketi, mnaona, simjui mwanamke huyu. Sijapata kumwona maishani mwangu, nijuavyo mimi, nasi hatufahamiani. Sina njia ya kujua. Kama hiyo ni kweli, ili kwamba tu watu wajue, inua mkono wako ili kwamba watu waone. Sasa je! tunaweza kuwa kama wale watu kule Sikari?

209 Sasa niangalieni. Ninamaanisha kama Petro na Yohana, walipopita kwenye lango linaloitwa Zuri. Sasa angalia.

210 Unaona, Yesu alivutia usikivu wake. Unaona? Yeye alijua ilibidi apande aende huko juu. Baba alikuwa amemtuma huko juu, bali Yeye hakujua. . .Mwanamke huyo akatokea, Naye akafikiri hiyo haina budi kuwa ndiyo. Unaona? Ndipo basi Yeye akamzungumzia mpaka akapata shida yake ilikuwa ni nini, ndipo akamwambia.

211 Hilo ndilo ninalofanya sasa hivi. Ni mimi nikijiondoa njiani, kusudi apate kuzungumza. Sasa, naam, ninaweza kuwaambia shida ya mwanamke huyu ni nini, kwa neema ya Mungu.

212 Shida yake ni, yeye ana vivimbe, na vivimbe hivyo viko kwenye tumbo. [Huyo dada anasema, "Ndiyo."—Mh.] Kweli kabisa. Je! unaamini ya kwamba Yeye ataviponya hivyo na kukupa afya? Wewe, je! unaamini hilo? Una mtu mwingine uliyekuwa ukiombea, pia, sivyo? Unaamini ataponya macho yake na kumfanya mzima, mvulana wako mdogo? Unaona, kwa kusema tu jambo hilo moja, kulielezea. Unaona? Vema. Nenda zako sasa, amini jambo hilo.

213 Hakulishika hapo kwanza, maana alikuwa ameshikilia hilo niani mwake. Niliona Nuru ikiendelea kumulika nyuma juu yake tena namna hiyo, kwa maana alikuwa akiombea jambo jingine. Na, lolote lile, hilo hapo. Unaona? Unaona?

214 Unaona, kama utaamini tu! Loo, laiti ungaliweza kulielezea! Sasa hilo linapaswa kumfanya kila mtu humu ndani. . .Mtu huyo mmoja tu, anapaswa kumfanya kila mtu aliye ndani humu aamini sasa hivi. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

215 U hali gani? Sasa sisi hatufahamiani, pia, nadhani. [Huyo dada anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Hatufahamiani. Sina fununu juu yako, kwamba wewe ni nani, kwamba unatoka wapi, ama—ama lolote juu yako. Lakini Mungu anajua habari zako. Sasa kama Yeye atanifunulia kwamba shida yako ni nini, je! utaamini kwamba mimi ni mtumishi Wake? ["Amina."]

Sasa, sasa iweni kimya mwezavyo kuwa.

216 Sasa, naam, una—una ugonjwa wa shinikizo la juu la damu, hiyo ni kweli, uliosababishwa na ugonjwa wa neva unaoifanya damu yako kuwa na presha. Na—na unachoka haraka sana, mara nyingi. Mtu mzuri sana, unaona. Unaona? Si anayekwenda kimkumbo; anaamini. Anaamini kweli kweli.

Naam, bwana. Nami—nami ninashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo. [Dada huyo anasema, "Niliomba nipate nguvu, Ndugu Branham."—Mh.]

217 Na, hebu, jambo lingine; kwa kuwa wewe ni mtu mzuri sana. Kwa kweli una familia kubwa. Mume wako ni mgonjwa, pia. [Huyo dada anasema, "Ndiyo."—Mh.] Yeye ana shinikizo la juu la damu, pia. ["Ndiyo."] Pia ana ugonjwa wa moyo. [Hiyo ni kweli."] Una mwana, naye ana ugonjwa wa moyo. Halafu una mmoja uliye na wasiwasi naye. ["Ndiyo."] Kuna kitu fulani cheusi. Mvulana huyo ametiwa uvuli. Yeye ni mlevi; yeye hunywa pombe. Na hiyo ni kweli. Sivyo? Endelea tu; ni sawa. Amini sasa. Endelea tu, nafikiri itakuwa sawa kama utaendelea tu na kuliamini.

218 "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio." Kama—kama unaweza kuamini ya kwamba yale Mungu aliyosema ni Kweli, hilo linatosha. Hivi hamdhani hayo ni kweli? Hiyo si ni Kweli? Hivyo sivyo alivyosema? Yeye aliahidi. Kwa hiyo, kama Yeye aliahidi, hilo linatosha. Alisema, "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana."

219 Sasa mnafikiri hao watu inawabidi kuwa—kuwa na hilo? Si lazima. Si lazima wawe wamesimama hapa jukwaani. Si lazima. Haiwabidi kuwa hapa, hata kidogo.

220 Yeye ana wakati mzuri sana huko nje. Na ninyi je! kwenye kusanyiko, mnaamini kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kila mmoja wenu?

221 Mama huyu anayeketi hapa akiniangalia, pale, ana ugonjwa wa moyo; amevaa nguo ya kahawia, nywele nyeusi, amevaa miwani. Una ugonjwa wa moyo. Mara tu ilipotajwa juu ya mama huyo hapo, kitu fulani kilikugusa. Hiyo ni kweli. Sasa uko mbali sana na mimi, bali uligusa Kitu fulani, sivyo? Je! sasa unaamini kwa moyo wako wote? Kama ukininii . . . Inua mkono wako, kama hiyo ni kweli. Vema.

222 Sasa hivi utanifanyia mema? Huyo mama anayeketi karibu na wewe, ambaye ameinua mkono wake pale, yeye ana ugonjwa wa shinikizo la juu la damu. Na kama ataamini kwa moyo wake wote, litamwacha, pia. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema.

223 Sasa niambieni kile walichogusa, kile walichogusa. [Kusanyiko linasema, "Yesu."—Mh.]

224 Je! unaamini Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa moyo, unayeketi pale, ukiomba, pia? Je! unaamini angeuponya moyo wako? Angeuponya kama ungemruhusu. Ninii tu, Yeye amefanya jambo hilo kama tu utaamini, bali kwanza huna budi kuliamini.

225 Huna budi kuamini. Unawajibika kuliamini, kwa maana hiyo ndiyo njia tu Mungu anayoweza kuponya. Je! unaamini hilo kwa moyo wako wote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

226 Mama huyu anayeketi hapa amevaa nguo nyeusi, ana shida ya shingo lake. Je! unaamini ya kwamba Mungu ataiponya, mama? Unaona? Unaona, haikubidi kuwa hapa juu jukwaani. Unaona?

227 Sasa angalia, mara tu ile Nuru ilipomwacha, ilirudi moja kwa moja; mama fulani alianza kulia, aliyeketi moja kwa moja nyuma yake. Mama aliyekuwa nyuma yake alianza kulia. Ilikuwa ni kitu gani? Alikuwa na hisia ngeni sana iliyomjia. Kama hiyo ni kweli, mama, uliye papo hapo nyuma yake, inua, inua mkono wako. Hiyo ni kweli, hisia ya ajabu sana ilikuja juu yako. Sasa, sababu ya hiyo kufanya hivyo, ni kwa sababu Yeye anataka kukuponya kutokana na ugonjwa huo wa tumbo, na kukufanya mzima. Je! unaamini ya kwamba Yeye atafanya hivyo? Amina. Unaona, kama tu utaamini, amini tu!

228 Mtu huyo anayeketi moja kwa moja pale akiniangalia akiwa mdadisi sana. Ni baridi yabisi. Anayeketi pale, mwishoni mwa kiti kule, je! unaamini ya kwamba Mungu atakuponya baridi yabisi hiyo na kukufanya mzima? Je! ungeamini? Mungu atakupa afya na kukuponya, kama unaweza kuamini.

229 Je! hivi huoni ya kwamba ni Yeye yule jana, leo, na hata milele? Hivi huwezi kuamini jambo hilo kwa ninii wako wote . . .

230 Vipi kama sikusema jambo lolote kwako? Unajua ninajua shida yako. Vipi kama sikusema jambo lolote, bali nilikuacha tu upite, ungeamini kwa moyo wako wote? Ninaamini uliponywa wakati ukisimama moja kwa moja pale. Kwa hiyo nenda tu, amini. Nenda, amini sasa, kwa moyo wako wote.

231 Je! unaamini ya kwamba Mungu alikuponya, na atamponya baba yako, pia, na kuwafanya nyote wawili wazima? Unafikiri atatoka hospitalini, akiwa na ugonjwa huo wa moyo? . . .? . . . Kama ukiamini! Unaona?

232 Kama utaamini tu, hivyo tu ndivyo unavyopaswa kufanya. Unaona? Hivi huoni kwamba ni Yeye? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

233 U hali gani, mama? Niangalie kwa dakika moja tu. Una udhaifu mwingi. Hiyo ni kweli. Mama yako ni mgonjwa, pia, hapa. Sivyo? [Huyo dada anasema, "Ndiyo."—Mh.] Ana ugonjwa wa moyo. Je! unaamini ya kwamba Mungu atamponya mama yako ugonjwa wake wa moyo? Hebu, jambo jingine, hebu kidogo, mume wako anaponywa shida hiyo ya tumbo, pia. Hebu, hebu kidogo, binti yako alikuwa na tatizo katika koo lake. Je! unaamini ya kwamba Yeye aliponya hilo pia? ["Ndiyo."] Naam, mjukuu wako ana kifafa, kama kuzimia, mtoto mchanga. Unaamini hicho kimeponywa, pia? Vema, nenda ukaamini.

234 Haleluya! Tunafanya nini? Kwa nini tusimwamini Yeye? Je! mko tayari kumwamini?

235 Basi hebu na tusimame kwa miguu yetu wakati Yeye anapoita, Roho Mtakatifu. Simameni na mumpe sifa, na mmwamini sasa hivi, kila mmoja wenu. Ninatamka ya kwamba Roho Mtakatifu yupo hapa, Biblia imetimizwa. Na katika Jina la Bwana Yesu Kristo, hebu kila—kila mmoja wenu ampe sifa sasa, nanyi mtaponywa. Amina.

SAUTI YA ILE ISHARA SWA64-0214
(The Voice Of The Sign)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, tarehe 14 Februari, 1964, katika ukumbi wa Mikutano wa Elliott huko Tulare, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2013 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org